# Nipashe

Jumamosi Julai 11, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580281

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Watu 13 mbaroni tuhuma mauaji ya watu 4 mgodini

UKURASA 3




UKURASA 11

# Mwinyi: Ulikuwa mtihani mgumu

**APITISHWA** kuwania urais Zanzibar, vigogo waonywa kuendekeza makundi... *Endelea ukurasa 2*




Dk. Hussein Mwinyi.tif

## MTIA NIA YA URAIS AAHIDI KUSUKA UPYA TAKUKURU

UKURASA 3



## Mzee Kinana aitwa Dodoma, wabariki Membe kufukuzwa

UKURASA 2


BAA LA CORONA



'USICHUKULIE POA UNATEGEMEWA'

* Nawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji tiririka
* Kaa kwa kuachiana nafasi hatua 2 au 3
* Vaa barakoa
* Ukikohoa au kupiga chafya ziba mdomo




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



MICHEZO SIMBA, YANGA KUMALIZA TAMBO UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

## Kinana aitwa Dodoma, Membe afukuzwa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

HALMASHAURI Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (NEC), imemsamehe Katibu Mkuu mstaafu wa chama hicho, Abdulrahman Kinana, na kumwondolea vizuizi alivyowekewa awali, huku ikibariki kufukuzwa uanachama kwa Benard Membe.

Kikao hicho kilifanyika jana chini ya Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais John Magufuli, kikihudhuriwa na wajumbe 166.

Akizungumza katika kikao hicho, Dk. Magufuli alisema Februari, mwaka huu, Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM, ilitoa adhabu kwa baadhi ya wanachama ambao walikiuka maadili na misingi ya chama.

"Nimeona nilichomeke hapahapa kwa kuwa ndiyo kikao cha uamuzi. Kwa hiyo, wajumbe wenzangu wa kamati kuu mnisamehe sana, lakini kubwa ni kwamba kikao kile kilitoa mapendekezo ya adhabu kwa baadhi ya wanachama wetu kutokana na misingi halali ya chama chetu.

"Lakini, hivi karibuni kama miezi minne mitano, mwenzetu mmoja ambaye ni Katibu Mkuu mstaafu (Kinana) alijitokeza hadharani kule Arusha na shahidi ni Mwenyekiti wa CCM Arusha, akaomba radhi, akajutia kwa kitendo alichofanya, kikubwa zaidi ndugu yetu aliomba radhi hadharani, ni kitendo ambacho ni kigumu watu wa kawaida kukifanya," alisema.

Dk. Magufuli alisema kitendo hicho kinahitaji nguvu ya Mungu kutubu hadharani, akibainisha kuwa aliguswa kwa kiwango kikubwa na kitendo hicho cha Kinana.

"Nina uhakika na ninyi wajumbe mliguswa sana, alikuwa amepewa adhabu ya miezi 18 na kalipio, na hakukataa kutumikia adhabu ile na hadi sasa ameshatumikia miezi kati ya minne au mitano.

"Niliona wajumbe wa NEC, chama chenye huruma na mapenzi mema, chama dume, niwaombe kama itawezekana kwa huruma yenu huyu ndugu yetu ambaye amekubali kutumikia adhabu yake hadi sasa tumsamehe," aliomba.

Kutokana na kauli hiyo, wajumbe wa kikao hicho walisikika wakisema "amesamehewa".

"Yule mwingine ambaye sitaki kumtaja, jina yeye ameshaondoka moja kwa moja, kwa hiyo adhabu ile si mnaikubali ya kumfukuza?" Dk. Magufuli aliuliza.

Aliwahoji wajumbe kuhusu hoja hiyo ambayo waliitikia "ndiyo" kuashiria kwamba wanakubaliana na uamuzi wa kumfukuza uanachama wa CCM aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Membe.

Wakati wa kuhitimisha hoja hiyo, Dk. Magufuli alitangaza kuwa Kinana amesamehewa rasmi kupitia kikao hicho na kumtaka ashirikiane na wana CCM kuchapa kazi huku akisisitiza CCM ni chama chenye huruma, upendo, kuzingatia maadili na miiko na kipo kwa ajili ya kuwatumikia Watanzania.

Dk. Magufuli pia alimkaribisha Kinana Dodoma ili ashiriki vikao vya juu vya uamuzi vya chama hicho vinavyoendelea leo jijini hapa.




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akitoa heshima za mwisho kwa mwili wa marehemu Balozi mstaafu Job Lusinde, alipofika nyumbani kwake, Uzunguni, jijini Dodoma jana. Wa pili kulia ni Waziri Mkuu mstaafu John Malecela. **PICHA: IKULU ZANZIBAR.**

# Mwinyi akiri ulikuwa mtihani mgumu

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameibuka mshindi katika kinyang'anyiro cha mgombea urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Licha ya kuibuka kidedea, mgombea huyo amekiri kuwa mchuano huo tangu kuanza mchakato wa kuchukua fomu, haukuwa kazi rahisi kwake ndiyo maana hata mwili umepungua.

Dk. Mwinyi aliibuka mshindi katika kura zilizopigwa na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM kwa kupata kura 129 sawa na asilimia 78.65 ya kura zote.

Akitangaza matokeo ya uchaguzi huo, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alisema Dk. Mwinyi aliwashinda Dk. Khalid Salum aliyepata kura 19 (asilimia 11.58 na Shamsi) Vuai Nahodha, kura 16 sawa na asilimia 9.75 ya kura zilizopigwa,

Baada ya Ndugai kutangaza matokeo hayo, Mwenyekiti wa CCM, Rais John Magufuli alisema kwa matokeo hayo wajumbe wameamua kwa hiari yao bila kulazimishwa wala kushurutishwa na mtu.

"Kwa upendo wenu ninyi wenyewe moyoni, kwa kumtanguliza Mungu wenu, kwa ajili ya ushindi mkubwa wa CCM Zanzibar na kwamba aliyechaguliwa mtakwenda kumtetea kwa nguvu zenu zote kwa ajili ya ushindi wa CCM na kwa masilahi mapana ya CCM. Dk. Hussein Mwinyi ndiye atakuwa mgombea urais wa Chama Cha Mapinduzi Zanzibar,"alisema.

"Dk. Mwinyi aliyeongoza kwa kupata kura asilimia 78.65 katika kura zote zilizopigwa hapa bila kuharibika hata kura moja ndiye aliyeteuliwa na kikao hiki cha Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM kupeperusha bendera ya Chama Cha Mapinduzi katika kinyang'anyiro cha urais wa Zanzibar," alisisitiza.

**ILIKUWA KAZI NGUMU**

Akizungumza baada ya kutangazwa mshindi, Dk.Mwinyi alisema ilikuwa kazi ngumu tangu kuanza kwa kinyang'anyiro hicho ndani ya CCM.

"Zoezi hili halikuwa rahisi. Katika maisha yangu nimefanya mitihani mingi lakini mkubwa kuliko yote ulikuwa huu. Ukiniona nimepungua sababu ni hili. Najua kazi iliyo mbele yangu ni kubwa lakini haitakuwa yangu peke yangu nitakuwa na ninyi.

"Ni kweli tulikuwa 32, kamati maalumu tulipatikana watano mimi nikiwemo. Nashukuru sana kwa hatua ile lakini baada ya pale, Kamati Kuu jana imeweza kutoa wagombea watatu na hatimaye leo nimepatikana mimi kama mgombea au mpeperusha bendera ya CCM katika nafasi ya urais Zanzibar. Hii ni heshima kubwa sana na kura nilizopata 129 ni nyingi sana. Hii inaonesha imani yenu juu yangu na mimi ninataka niwaahidi kwamba nitafanya kazi. Nitalitumika taifa hili kwa uwezo wangu wote," alisema.

"Kinachonipa faraja ni kwamba pamoja na kwamba tulikuwa 32 na hatimaye niko mimi wenzangu wote wako tayari kushirikiana nami,"

Awali, akiomba kura, Dk. Mwinyi aliahidi endapo atachaguliwa, ataenzi Mapinduzi ya Zanzibar na kudumisha Muungano na kuyaendeleza yale yote mazuri yaliyofanywa na Rais Dk. Ali Mohamed Shein.

"Vilevile niwaahidi nitatekeleza kwa vitendo Ilani ya CCM mwaka 2020 hadi 2025 itakayotolewa kwa upande wa Zanzibar. Kwa heshima na taadhima na kwa unyenyekevu mkubwa naomba mnipigie kura nyingi za ndiyo mimi Hussein Ali Mwinyi," alisema.

**JMP NA MBELEKO**

Kabla ya kuanza kupigwa kura na baada ya wagombea watatu kumaliza kujieleza, Rais John Magufuli alimtaka Dk. Shein kutoa neno kwa kuwa katika kampeni mtu anaweza kusema ametumwa na fulani.

"Mtu anaweza kusema nimetumwa na huyu, huyo chaguo la fulani. Mimi walikuwa wanasema chaguo langu ni (Prof. Makame) Mbarawa nimemleta nimembeba. Sasa sifahamu leo watazungumza nani. Kura zitapigwa humu na kuhesabiwa hapa hapa," alisema.

Aliwaambia wajumbe kwamba kinachohitajika ni ushindi katika uchaguzi mkuu na si kwenda kujaribu kushinda, hivyo kuwataka kumchagua mtu atakayekwenda kushinda. Alisema katika dhamira zao kila mmoja ajitafakari atakayemchagua na ushindi lazima upatikane.

**KAULI YA PROF.MBARAWA**

Akizungumza miongoni mwa wagombea walioingia katika majina matano, Prof. Makame Mbarawa alishukuru chama kwa kumpa heshima ya kuwa miongoni mwa waliochukua fomu huku akisema safari hiyo haikuwa rahisi.

"Tulikuwa wengi, tulipita kwenye milima na mabonde mengi, maneno mengi mazuri na mabaya lakini leo jahazi yetu imefika bandarini na lengo letu ni moja tu CCM kupata ushindi,"alisema.

Aliongeza "Naomba nikuhakikishie Mwenyekiti yule ambaye leo hii atakuwa mshindi huyo ndo atakuwa mshindi wetu na Rais Zanzibar, mimi saa zote wakati wote nitatoa muda wangu kumhudumia yeye ili kupata ushindi."

Dk. Shein, ambaye ameongoza Zanzibar kwa miaka 10 na anamaliza muda wake, aliposimama alisema hajambeba mtu yeyote kati ya wanachama waliojitokeza kutaka kumrithi.

"Mimi sijawa na mgombea na sitakuwa na mgombea. Sijambeba mgombea, sijapata kufanya hivyo. Kila mwanachama ana haki ya kugombea CCM. Yasitangazwe ambayo hayapo, najua yamesemwa kwamba Hamisi Mussa chaguo la Rais na jana tumesikia Rais kasemwa anambeba Mbarawa, na mimi sijambeba Mussa, muulizeni na wala sitafanya hivyo," alisema Dk. Shein.

Alisema ameyasema hayo waziwazi kwa kuwa wengine hupenda kuhusisha kuwa viongozi wa juu wana watu mtu wao wamemweka mfukoni watamtoa.

"Kwa mimi mfuko wangu wa shati haingii Bwana Hamis Mussa. Watafute mengine waseme waliyotaka kusema wasiseme hili. Ana haki yake na chama hiki, kachukua fomu kajaza, kapita alikopita Kamati Kuu haikumpitisha. Tusihusishwe sisi bure, mimi sijawahi kuhusishwa tangu niwe kwenye chama, hebu tuwe waungwana. Tuseme yale tunayotakiwa kusema," alisema.

## HABARI KITAIFA



Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu, Mariam Mmbaga (wa pili kushoto), akipokea vifaa kinga vya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona vyenye thamani ya Sh. milioni 23.7 kutoka kwa Mratibu wa shirika la Amref Health Afrika, Gaspery Misungwi, mjini Shinyanga, jana. Kushoto ni Mganga Mkuu wa mkoa huo, Dk. Khamis Kulemba. **PICHA: HAPPY SEVERINE**

# Mtia nia ya urais aahidi kuisuka upya TAKUKURU

**Na Mary Geofrey**

WAKILI wa Mahakama Kuu, Simba Richmomd Akaro, amechukua fomu ya kuomba kuteuliwa kuwania urais wa Tanzania kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), akiahidi kusuka upya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) endapo atafanikiwa kukalia kiti hicho.

Wakili Simba alikabidhiwa fomu hiyo jana kwenye Ofisi za Makao Makuu ya CHADEMA jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa chama hicho, Reginald Munisi.

Baada ya kukabidhiwa fomu hiyo, Wakili Simba alitaja mambo atakayoyafanya endapo atapitishwa na CHADEMA kugombea nafasi hiyo na kushinda kuwa ni pamoja na kuboresha vyombo vinavyosimamia haki. Alisema uboreshaji huo utaigusa moja kwa moja TAKUKURU ambayo kwa mtazamo wake anaona kwa sasa haiko huru katika kupambana na wala rushwa nchini.

Vilevile, Wakili Simba alisema akifanikiwa kupitishwa na CHADEMA kugombea urais wa Tanzania kisha kuchaguliwa na Watanzania kuwaongoza, atahakikisha maendeleo na demokrasia vinaenda pamoja.

"Tusiwe tunaongelea maendeleo bila demokrasia. Ukiwa na moja tu ni ulemavu, ni muhimu kwamba demokrasia na maendeleo viwe vinakwenda sambamba," alisema.

Aliishauri CHADEMA kutowapa nafasi ya kuwania nafasi mbalimbali za uongozi kupitia chama hicho, wanasiasa walioshika nafasi za uongozi serikalini kwa muda mrefu, kwa maelezo kwamba wamechokwa na wananchi.

Wakili Simba anakuwa mtia nia wa sita ndani ya CHADEMA kuchukua fomu ya kuomba kuteuliwa kugombea urais kupitia chama hicho katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu tangu kuanza kwa mchakato huo Julai 4, ukitarajiwa kufungwa Julai 19 mwaka huu.

Waliochukua fomu awali ni Makamu Mwenyeketi wa chama hicho, Tundu Lissu, Dk. Mayrose Majinge, Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kati, Lazaro Nyalandu, Wakili Gaspar Mwalyela, aliyekuwa Meya wa wa Jiji la Dar es Salaam, Isaya Mwitta na Leonard Manyama, aliyechukua fomu juzi jioni.

# Mbaroni tuhuma za mauaji mgodini

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MKUU wa Operesheni Maalum za Jeshi la Polisi, Kamishna Liberatus Sabas, amezitaka mamlaka zinazoshugulikia utoaji wa nyaraka na vibali vya kusafirisha mchanga wa dhahabu, kujiridhisha kuhusu uhalali wa mchanga huo kwa kufika kwenye eneo unakotolewa.

Vilevile, amesema watu 13 wanashikiliwa na jeshi hilo kwa tuhuma za kuhusika na mauaji ya watu wanne eneo la uchenjuaji dhahabu wilayani Kahama mwishoni mwa mwezi uliopita.

Mihayo Msikhela amesema kuna haja wahusika kujiridhisha unakotoka mchanga huo na kumbaini mmiliki halali wa eneo au mchanga husika, ili kueupuka kutoa vibali kwa mchanga uliopatikana kwa njia ya uhalifu na kuikosesha mapato serikali.

Alitoa rai hiyo juzi alipowasilisha taarifa kuhusu tukio la mauaji ya watu wanne yaliyofanyika katika Mgodi wa Wachimbaji Wadogo Tambalale Na. 4 ulioko Kijiji cha Wisolele, Kata ya Segese wilayani Kahama.

Msikhela alisema kuwa katika tukio hilo lililotokea Juni 30, mwaka huu majira ya saa mbili usiku kwenye eneo la kuchenjua dhahabu, watu wanne waliuawa kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali maeneo ya kichwani na watu wasiojulikana.

Kiongozi huyo aliwataja waliouawa katika tukio hilo kuwa ni: Juma Jigwasanya (42), mlinzi wa Kampuni ya Sekepa na mkazi wa Nundu, Nyang'hwale; Lusajo Mwamasangula (31), mlinzi wa Kampuni ya Sekepa na mkazi wa Tine; Raphael Mapinduzi (27), mwendesha mitambo huo na mkazi wa Katoro, Geita; na Daniel William Mapunda (25), msimamizi wa mtambo na mkazi wa Geita.

Alisema kuwa katika tukio hilo, Exavery Maulid (21), mwendesha mitambo, alinusurika kifo baada ya kujeruhiwa kwa kugongwa na kukatwa na kitu chenye ncha kali kichwani kisha kuwekwa pamoja na miili ya marehemu, wahusika wakiamini tayari alikuwa ameshapoteza maisha.

Alisema kuwa baada ya tukio hilo, Jeshi la Polisi kwa kushirikina na vyombo vingine vya ulinzi na usalama pamoja na wananchi, walianza msako wa kuwatafuta wahalifu hao na kufanikiwa kuwakamata wahalifu 13 wakiwa na vielelezo mbalimbali na kuongeza kuwa baada ya upelelezi kukamilika, watafikishwa mahakamani.

Alisema kuwa uchunguzi wao umebaini kuna kundi la uhalifu lililopanga mpango huo wa mauaji na lilitekeleza uhalifu na mauaji hayo kisha kusafirisha na kuhifadhi mzigo huo baada ya wizi kufanyika.

Alibainisha kuwa baadhi ya vielelezo vilivyokamatwa ni mchanga wenye Carbon iliyonasa dhahabu, viroba saba ulioibwa katika mtambo siku ya tukio ukiwa na uzito wa kilogramu 385.34, makapi ya mchanga wenye kaboni ukiwa na uzito wa kilogramu 465.76 uliokutwa umefichwa katika nyumba ya mmoja wa watuhumiwa ukiwa pamoja na viroba saba vya mchanga wenye kaboni iliyoibwa siku ya tukio.

Vielelevyo vingine ni pikipiki tano ikiwamo iliyotumika kubeba huo mzigo na nyingine moja ambayo mtuhumiwa alikimbia na kuitelekeza kwenye nyumba aliyokuwa akilinda viroba vya Carbon iliyokuwa imeibwa.

Vingine bunduki aina ya shortgun yenye namba 9025817 iliyoporwa kwa mlinzi mmoja wapo aliyeuawa siku ya tukio ikiwa na risasi mbili na baadaye kutelekezwa umbali wa mita 400 toka eneo la tukio. Pia panga lenye vimelea vya damu.

**NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kampuni ya **WAUNGWANA AUCTION MART na SUMA JKT AUCTION MART** kwa niaba ya AccessBank Tanzania Limited watauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba, Magari na Viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kuwa utakapopita muda uliopangwa tangu kutoka kwa gazeti hili. Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada. Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| S/N | TAWI HUSIKA | KAMPUNI INAYO HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 01 | LUMUMBA | WAUNGWANA AUCTION MART | MTUI/GERVAS,CALVIN | MTUI/GERVAS,C ALVIN | KIWANJA | VIKINDU | 27/07/2020 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 02 | LUMUMBA | WAUNGWANA AUCTION MART | MUYENGI/K,LESBONETH | MUYENGI/K,LES BONETH | NISSAN CIVILIAN T 357 CTT | KIJICHI | 19/07/2020 SAA 4: 00 ASUBUHI |
| 03 | LUMUMBA | SUMA JKT AUCTION MALT | ONE PLANET SCHOOLS LIMITED | MAHIGA/JULIUS, ELIZABETH | COASTER 837 DPQ | DODOMA | 27/07/2020 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 04 | LUMUMBA | SUMA JKT AUCTION MALT | MAHENDE/ALPHONCE,E STHER | MAHENDE/ALPH ONCE,ESTHER | KIWANJA NA NYUMBA | KIFURU | 27/07/2020 SAA 4:00 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa mara usomapo tangazo hili.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa malipo ya 25% ya fedha taslimu papo hapo na 75% baada ya siku 14 toka siku ya mnada kufanyika na ukishindwa kulipa malipo yaliyobaki mnada utarudiwa na fedha ulizo lipa hazitarudishwa.
3. Gharama za kubadilisha umiliki ni za mnunuzi mwenyewe, kumbuka vigezo na masharti kuzangatiwa.

**MAWASILIANO**
**WAUNGWANA AUCTION MART 0713077474**
**SUMA JKT 0712407883**

# JPM ateua Wakili Mkuu, DC

**Na Mwandishi Maalum**

RAIS John Magufuli amemteua Gabriel Malata kuwa Wakili Mkuu wa Serikali huku akifanya pia uteuzi wa mkuu wa wilaya na mkurugenzi mtendaji wa wilaya.

Kabla ya uteuzi huo, Malata alikuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali na anachukua nafasi ya Dk. Julius Mashamba.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Rais Magufuli pia amemteua Dk. Boniface Luhende kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali.

Kabla ya uteuzi huo, Dk. Luhende alikuwa Mhadhiri katika Shule Kuu ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na anachukua nafasi ya Malata ambaye ameteuliwa kuwa Wakili Mkuu wa Serikali.

Ilielezwa katika taarifa hiyo ya Ikulu kuwa uteuzi wa viongozi hao ulianza jana.

Rais Magufuli pia amemteua Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Advera Bulimba kuwa Mkuu wa Wilaya ya Nzega mkoani Tabora. Kabla ya uteuzi huo, Advera alikuwa Kamanda wa Kikosi cha Polisi TAZARA na anachukua nafasi Godfrey Ngupula.

Vilevile, Rais Magufuli amemteua Solomon Shati kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang mkoani Manyara. Kabla ya uteuzi huo, Shati alikuwa Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe mkoani Katavi na anachukua nafasi ya Bryceson Paul Kibasa.

Wakati huo huo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kapteni mstaafu George Mkuchika, kwa mamlaka aliyokasimiwa na Rais wa Tanzania, amefanya uteuzi wa makatibu tawala wa wilaya mbili.

Waziri huyo amemteua Omary Mwanga kuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi. Mwanga anachukua nafasi ya Husna Juma Sekiboko.

Pia, amemteua Saitoti Stephen kuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbeya mkoani Mbeya. Kabla ya uteuzi huo, tephen alikuwa Ofisa Tarafa wilayani Mbulu mkoani Manyara na anachukua nafasi ya Hassan Mkwawa. Uteuzi wa viongozi hao ulianza juzi.

# Waziri Lukuvi apokea msaada wa kompyuta

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amepokea msaada wa kompyuta 10 zenye thamani ya milioni 12 kutoka Benki ya Azania.

Msaada huo ulipokewa jana katika Ofisi za Ardhi Mkoa wa Dodoma na kushuhudiwa na viongozi mbalimbali wa wizara akiwamo Katibu Mkuu, Mary Makondo.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Waziri Lukuvi aliishukuru Benki ya Azania kwa msaada huo alioueleza kuwa utasaidia kwenye huduma za sekta ya ardhi, hasa katika ofisi za ardhi za mikoa zilizoanzishwa hivi karibuni.

Alisema Benki ya Azania imekuwa ikiunga mkono jitihada za wizara kusaidia vifaa na kuzitaka taasisi nyingine kuiga mfano wa benki hiyo kusaidia juhudi za serikali kusogeza huduma za ardhi karibu na wananchi.

Kwa mujibu wa Lukuvi, hivi sasa wizara yake baada ya kuanzisha ofisi za ardhi katika mikoa, inafanya jitihada mbalimbali kuhakikisha ofisi hizo zinakuwa na vifaa vya kutosha kwa lengo la kuwawezesha watendaji wa ofisi hizo kufanya kazi kwa ufanisi.

Meneja wa Benki ya Azania Mkoa wa Dodoma, Makalla Mbura, alimweleza Waziri Lukuvi kuwa msaada uliotolewa, ni moja ya juhudi za benki hiyo kusaidia jitihada mbalimbali zinazofanywa na wizara kwenye sekta ya ardhi.

Makalla aliongeza kwa kusema kuwa, benki hiyo itaendelea kuunga mkono jitihada za wizara katika masuala mbalimbali ya huduma za sekta ya ardhi kwa kutoa msaada pale unapohitajika




Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof Ibrahim Juma, akizungumza kwenye sherehe za 62 za kuwapokea na kuwakubali mawakili wapya zilizofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Jaji Mkuu awafunda mawakili wapya

**Na Hellen Mwango**

JAJI Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma, amewataka mawakili wapya 601 wa kujitegemea, kujihusisha na shughuli zingine za kiuchumi ikiwamo kilimo na ufugaji badala ya kutegemea kazi ya uwakili pekee.

Pia amewataka kuisoma Dira ya Taifa ya Maendeleo inayoeleza kwamba karne ya 21 ni ya ushindani.

Prof. Juma alitoa rai hiyo jana katika viunga vya Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wakati akiwapokea na kuwakubali kwa njia ya video mawakili hao waliokuwa wakifuatilia matangazo ya moja kwa moja kupitia Televisheni ya Taifa.

"Wengi hawajui Dira ya Taifa ya Maendeleo, wengi niliongea nao walisema hawajui dira inaelekea wapi, nawashauri ninyi mawakili mkajihusishe na shughuli za kiuchumi ikiwamo kilimo, mifugo na biashara badala ya kutegemea kazi ya uwakili pekee," alisema Prof. Juma.

Alisema pamoja na kujihusisha na shughuli za kiuchumi, ili kuendana na soko la ushindani, ni lazima wajikite kwenye matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TAHAMA) kwa kuwa mahakama inaandaa kanuni zitakazoanzisha mfumo wa kusajili kesi mbalimbali na kusikiliza kwa njia ya mtandao.

Alisema mawakili wengi bado wanakosa kazi za kudumu kutoka kampuni mbalimbali za uwakili, taasisi za umma na serikali kwa sababu kazi za kiwakili zimepungua kwa kuwa dunia ya sasa ya teknolojia ni ya kujichanganya katika fursa mbalimbali.

Jaji Mkuu alisema kipindi cha miezi mitatu ya kujilinda na virusi vya homa ya mapafu ya corona, mahakama nchini imesikiliza kesi 3,874 kwa njia ya mtandao wakati mahabusi wakiwa katika magereza husika.

Kuhusu maadili, Jaji Mkuu alisema mawakili hawana budi kuheshimu usiri kati yao na wahitaji wa huduma ya kufatuta haki ikiwamo kutunza siri bila kusahau kujifunza taaluma zingine.

Naye Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Prof. Adeladus Kilangi, aliwaasa mawakili hao kuacha kujihusisha na vitendo vya kughushi nyaraka ikiwamo za mirathi kwa kuwa wajibu wao ni kusimamia haki kwa jamii.

Alisema tume ya maadili imekuwa ikipokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kuhusu mawakili kujihusisha na jinai kwa makusudi hali inayosababisha jamii kukosa imani nao.

Kwa Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Dk. Lugemeleza Nshala, alisema hiyo ni awamu ya 62 na ya kwanza ya mawakili 601 kuapishwa kwa njia ya mtandao na kwamba wanapaswa ni kuyazingatia na kuyafanyia kazi maarifa waliyopewa.

Alisema majukumu yao kama mawakili ni kusimamia haki na kwamba bila nchi kuendeshwa kwa misingi ya sheria kumekuwa na uonevu mkubwa katika jamii.

HABARI KITAIFA

# Milioni 7 kunufaika mpango wa TASAF

**Na Welingtone Masele,** SIKONGE

ZAIDI ya watu milioni saba wanaotoka katika kaya maskini nchini, wanatarajiwa kunufaika na mpango wa serikali wa kuwezesha kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Hayo yalibainishwa jana na Ofisa wa Mfuko huo kutoka Makao Makuu, Grace-Anna Maganga, alipokuwa akifungua mafunzo ya siku nne ya kuhakiki taarifa za wanufaika wa mpango huo kwa wasimamizi wilayani Sikonge kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Ladislaus Mwamanga.

Alisema kipindi cha pili cha awamu ya tatu (TASAF III) ya mpango huo, kinatarajia kufikia kaya maskini milioni 1,450,000 zenye zaidi ya watu milioni saba katika vijiji na mitaa ya halmashauri zote nchini ili kuboresha hali zao kiuchumi.

Maganga alibainisha kuwa mkazo mkubwa katika awamu hii utakuwa kuwezesha kaya zote zitakazoandikishwa kufanya kazi ili kujiongezea kipato ikiwamo kuongeza na kuboresha huduma za kijamii katika halmashauri zote 187 zilizopo nchini.

Kwa wa Maganga, mafunzo hayo yamelenga kuwapa mbinu za uhakiki wa walengwa wa mfuko huo utakaofanyika nchini kote ili kuondoa kaya zote za walengwa ambazo zimepoteza sifa.

"Utekelezaji wa mfuko huo katika awamu ya kwanza umepunguza umaskini wa mahitaji ya msingi kwa kaya kwa asilimia 10 na umaskini uliokithiri pia umepungua kwa asilimia 12," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya hiyo, Peresi Magiri, alipongeza serikali kwa kuanzisha awamu ya pili ya mpango huo kwa kuwa utasaidia kuboresha maisha ya wananchi wanaotoka katika familia maskini wilayani hapa.

Aliongeza kuwa, katika awamu ya kwanza ya mpango huo, vijiji 46 kati ya 71 vilivyoko katika wilaya hiyo vilinufaika lakini awamu hii ya tatu vijiji vyote nchini, ikiwemo vya Sikonge, vitanufaika.

Mratibu wa TASAF wilayani Sikonge, Claud Nkanwa, alisema uhakiki wa walengwa umekuja wakati mwafaka kwa kuwa kaya maskini nyingi zimekuwa zikilalamika kutoingizwa katika mpango wakati zilistahili.

Aliongeza kuwa awamu ya pili ya mpango huo ni mkombozi kwa wakazi wa wilaya hiyo kwa kuwa utasaidia kuinua kaya maskini kiuchumi ikiwamo kutoa ajira za muda mfupi kwa makundi mbalimbali ya kijamii yenye hali duni kimaisha.

# Tanzania, China zaahidi kuendeleza ushirikiano

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA na China zimeahidi kuendeleza ushirikiano wa kidiplomasia ili kuhakikisha pande zote zinakuwa na maendeleo endelevu.

Makubaliano hayo yalifanywa na Balozi wa China nchini, Wang Ke, wakati alipokutana kwa mazungumzo na Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, jana jijini Dar es Salaam.

Balozi Ibuge alisema wamejadiliana masuala mbalimbali ikiwamo namna ya kutekeleza nia ya viongozi wakuu wa Tanzania, Rais John Magufuli na Rais wa China, Xi Jinping, ya kupunguza madhara yatokanayo na ugonjwa wa COVID19 ikiwamo kufutiwa na kusamehewa madeni.

"Naishukuru serikali ya China kwa uhusiano na ushirikiano ambao imekuwa ikionyesha kwa Tanzania. Uhusiano huo umeendelezwa na viongozi wa pande zote mbili ambao umekuwa ukiimarika siku hadi siku na serikali ya Tanzania itaendelea kudumisha ushirikiano wa kidiplomasia kati yake na China.

Pamoja na mambo mengine, mazungumzo yalihusu masuala ya biashara na uwekezaji, mradi wa nyumba 25 za wataalum wa afya zilizoko Osterbay, jijini Dar es Salaam.

Balozi Wang Ke, pamoja na mambo mengine, aliipongeza serikali ya Tanzania kwa jitihada ilizochukua katika kukuza uchumi wake hadi kufikia uchumi wa kati pamoja na mapambano dhidi ugonjwa wa corona.

"Leo (jana) nimekutana na Katibu Mkuu wa Mambo ya Nje, Balozi Ibuge na kuzungumza mambo mbalimbali ya ushirikiano. Tunaipongeza serikali ya Tanzania kwa jitihada ilizochukua katika kufanya kazi kwa bidii na kukuza uchumi wake hadi kufikia uchumi wa kati pamoja na hatua ilizochukua katika kupambana na janga la COVID 19 ambapo tumefurahishwa kuona janga hili limeisha," alisema Balozi Ke.

Balozi Ke aliongeza kuwa wamekubaliana katika mazungumzo hayo pia kuendeleza ushirikiano wa kufanya kazi kwa pamoja kwa manufaa ya pande zote ili kuhakikisha uhusiano na ushirikiano unazidi kukua na kuimarika.

Tanzania na China zimekuwa zikishirikiana katika sekta za kilimo, biashara na uwekezaji, miradi ya mikopo nafuu na misaada, teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), uchukuzi, afya, utalii na utamaduni.

China na Tanzania zilianzisha rasmi uhusiano wa kidiplomasia mwaka 1964.




Mkuu wa Wilaya ya Monduli, mkoani Arusha, Edward Balele, akizungumza na wafanyabiashara baada ya kufanya ziara ya kushtukiza katika soko la Alhamisi, mjini Monduli, kukagua zoezi la ugawaji wa vitambulisho vya machinga sokoni hapo juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Dk. Shein amlilia Balozi Lusinde

**Na Mwandishi Wetu,**

DODOMA

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ametoa mkono wa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa Balozi Mstaafu Job Lusinde, aliyefariki dunia Jumanne wiki hii.

Dk. Shein alifika nyumbani kwa marehemu jana asubuhi, Uzunguni jijini hapa na kutoa mkono wa pole kwa familia pamoja na kumpa pole mjane Sara Lusinde.

Akitoa mkono wa pole, Dk. Shein alieleza alivyoguswa na kifo cha aliyekuwa mmoja wa mawaziri 11 wa kwanza wa serikali ya Tanganyika na kusisitiza kwamba kiongozi huyo mkongwe wa siasa atakumbukwa kwa mchango wake mkubwa akiwa waziri, balozi, mdhamini wa CCM na kiongozi wa wazee wa Dodoma.

Rais Dk. Shein alipata fursa ya kuuaga mwili wa Marehemu Balozi Lusinde akiwa pamoja na ndugu, jamaa, marafiki na viongozi mbalimbali nyumbani kwake.

Bada ya kufika nyumbani kwa marehemu, Dk. Shein alitia saini kitabu cha maombolezo akimwomba Mwenyezi Mungu awape subira na aiweke roho ya marehemu mahala pema peponi.

Akitoa neno la shukrani, Waziri Mkuu Mstaafu John Malecela, ambaye ni mdogo wa marehemu, alimshukuru Dk. Shein kwa kushiriki kikamilifu katika msiba huo na hatimaye kuuaga mwili wa marehemu.

Mwanasiasa huyo mkongwe, Balozi Job Lusinde (90) alikuwa mmoja wa viongozi katika Baraza la Kwanza la Mawaziri baada ya uhuru, alifariki dunia katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili jijini Dar es Salaam.

Familia ya Balozi Lusinde na Malecela ilieleza kuwa taratibu za mazishi zinaendelea na jana asubuhi mwili wa marehemu ungepelekwa kanisani kwa ajili ya kuendelea na taratibu za mazishi. Lusinde alikuwa kaka Mzee Malecela.

Balozi Lusinde alizaliwa Oktoba 9, 1930 na aliwahi kuwa Waziri wa Mawasiliano mwaka 1965 na ni miongoni mwa watu waliofanya kazi kwa karibu na Mwalimu Julius Nyerere akiwa Waziri wa Serikali za Mitaa mwaka 1961.

Pia aliwahi kuwa Balozi wa Tanzania nchini China kuanzia mwaka 1975 hadi mwaka 1984 pamoja na kuwa Balozi wa Tanzania nchini Kenya.

Balozi Lusinde alikuwa ndiye kiongozi pekee aliyekuwa amebaki hai miongoni mwa Mawaziri wa Baraza la Kwanza la Mawaziri wa Serikali ya Awamu ya Kwanza iliyoongozwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

Mwili wa kiongozi huyo ulitarajiwa kuzikwa jana katika makaburi ya Kikuyu jirani na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohana, jijini Dodoma.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waamuzi Simba, Yanga mjiepushe na upendeleo

**WATANI** wa jadi nchini, Simba na Yanga zote kutoka jijini Dar es Salaam, zinatarajia kukutana kesho Jumapili kwenye Uwanja wa Taifa katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA.

Bingwa wa michuano hiyo, hupata tiketi ya kuiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika ambayo huandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Yanga ndio ilikuwa timu ya kwanza kutinga katika hatua hiyo baada ya kuwafunga Kagera Sugar mabao 2-1 huku Simba yenyewe iliwachapa magoli 2-0, waliokuwa mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Azam FC.

Simba itashuka katika mashindano hayo yanayochezeshwa kwa mfumo wa mtoano ikiwa tayari na tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kutetea taji la Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kwa maana hiyo, Yanga ambayo haina tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa mpaka sasa, itaingia uwanjani ikifahamu wazi kushinda mechi hiyo kutaifanya isonge mbele katika mashindano hayo ili kuwania kombe hilo na endapo itashinda, itakuwa imepata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa.

Mshindi wa nusu fainali hiyo, atakutana na mshindi wa mechi nyingine kati ya Sahare All Stars ya jijini, Tanga dhidi ya Namungo FC kutoka mkoani Lindi.

Yanga, ambayo inafundishwa na Mbelgiji, Luc Eymael ndiyo inaonekana wazi kuhitaji zaidi tiketi ya kushiriki mashindano ya CAF, kuliko timu nyingine ili kuwatuliza mashabiki wake baada ya kushindwa kutwaa taji la Ligi Kuu Bara kwa msimu wa tatu.

Katika siku za hivi karibuni, waamuzi wameonekana kuchangia kuchezesha chini ya kiwango au kuchezesha kwa 'mahaba' na timu mojawapo, jambo ambalo limeamsha hasira na malalamiko kutoka kwa wadau wa mchezo huo hapa nchini.

Wakati mwingine uamuzi huo usioridhisha umekuwa ukichangia kupata matokeo ambayo yanaumiza timu mojawapo na hali hii inaleta taswira mbaya katika maendeleo ya mchezo huu wenye mashabiki wengi hapa nchini na duniani kwa ujumla.

Nipashe inapenda kuwakumbusha waamuzi watakaopata dhamana wa kuchezesha mechi hii kufuata kikamilifu kanuni za mchezo huu kwa kuamua kulingana na tukio husika.

Kwa kufanya hivi, mwisho wa mchezo, timu itakayostahili kushinda ndiyo ishinde na si kuanzisha mjadala mwingine baada ya filimbi ya mwisho kumalizika.

Uamuzi mbaya wa kiwango cha chini au ya upendeleo yamekuwa yakiacha 'vidonda' kwa timu na matokeo yake upande usiostahili umekuwa ukifaidika na uchezeshaji huo, ambao huondoa maana halisi ya maandalizi na uwekezaji katika klabu.


Gazeti hili tunawakumbusha waamuzi watakaopewa dhamana kuchezesha kwa weledi, umakini na haki ili timu itakayotumia vema nafasi zake kumaliza mechi hiyo kwa kicheko badala ya kuwasilisha malalamiko katika Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), ambayo hayatabadilisha matokeo ya uwanjani.

Tunakumbusha kuwa, Namungo na Sahare pia wanahaki ya kuiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa, hivyo timu mojawapo ikifanikiwa kuingia katika fainali, itendewe haki na waamuzi hao.

Inafahamika, waamuzi wanaoboronga wanafungiwa, lakini adhabu hii haisaidii timu ambayo ilionewa uwanjani kwa sababu haipati nafasi ya kupewa kile ilichodhulumiwa huku mashabiki nao tunawakumbusha kuwa na nidhamu wakati wote wa mchezo huo.

Tunasema haya kwa sababu tunataka kuona Tanzania Bara inapata mwakilishi sahihi katika mashindano ya kimataifa na kusahau tabia za kupendelea baadhi ya timu kwa kigezo cha kuridhisha wachache au maslahi ya upande usiostahili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Kongole Ali Mayai kwa hilo



Na Barnabas Maro

**MTU** anapofanya jambo zuri anastahiki tuzo/tunzo. Maana ya 'kongole' ni shukrani; asante. 'Tuzo/tunzo' maana yake ni zawadi anayopewa mtu kwa kufanya jambo jema au kazi nzuri.

Stahiki ni kitendo cha mtu kuwa na haki ya kupata kitu fulani kutokana na ufanisi aliopata. Ali Mayai anastahiki kupewa zawadi kwa kazi nzuri aliyofanya. Imebidi nieleze maana ya neno 'stahiki' ili wanaopitia makala na wasomaji wasidhani nimekosea kutumia neno hilo kwamba neno sahihi ni 'stahili,' hapana.

'Stahili' ni kitendo cha mtu kupata adhabu kulingana na jambo baya alilofanya. Kwa mfano, "mwafulani (jina linalotumika kumtaja mtu ambaye yupo lakini jina lake linafichwa) anastahili adhabu kwa kitendo alilofanya."

Turudi kwenye mada (jambo linalozungumzwa, kusomeshwa au kuandikwa). Muungwana (mtu mwenye tabia njema), Ali Mayai aliyekuwa mchezaji mahiri wa Yanga kabla ya kustaafu, aliandika makala kwenye gazeti maarufu la michezo nchini iliyopewa kichwa: "Timu zijengwe kisayansi, badala ya kukurupuka."

Amezitaja zaidi timu za Simba na Yanga na mashabiki ambao wamekuwa na tabia ya kutwaa ubingwa kwa kubadilishana. Kwamba mashabiki wa timu hizo kudhani kuwa ndizo zenye wajibu wa kuiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya kimataifa!

Nauliza: Kama Ligi Kuu ina timu 20, kwa nini Simba na Yanga zionekane ndizo zinazofaa kuiwakilisha Tanzania Bara kwenye michuano ya kimataifa? Timu 18 zilizobaki hazitaki kuiwakilisha nchi kwenye michezo ya kimataifa au zimeamua kuwa wasindikizaji?

Mayai anatoa mfano wa baadhi ya mechi ambazo Simba na Yanga hucheza na timu zingine katika ligi na kutawaliwa katika maeneo yote ingawa kuna wakati timu hizo hufanikiwa kupata matokeo tu kwani wachezaji wao huwa na mizigo ya fikra vichwani mwao.

Mfano mzuri ni mechi ya Kagera Sugar na Yanga iliyochezwa Jumatano ya wiki hii na Yanga kushinda bao 1-0 kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba. Niliangalia mechi ile mwanzo mpaka mwisho na kusikitishwa mno kwa jinsi Yanga ilivyocheza.

Ingawa Yanga ilishinda, nina kila sababu ya kusifu uchezaji wa Kagera Sugar licha ya kushindwa kwani katika mchezo kuna kushinda na kushindwa. Nathubutu kusema Yanga ilipata bahati ya kuishinda Kagera iliyomiliki mpira kuliko Yanga walioonekana kuwa kama wanafunzi wa kandanda!

Nakubaliana na methali ya wahenga kwamba: "Bahati humwacha wa mbele na kumfuata wa nyuma." Maana yake bahati huweza kumwendea mtu yeyote. Methali hii hutumiwa hasa pale ambapo bahati imemwangukia mtu ambaye hakutarajiwa.

Kagera Sugar chini ya mwalimu wao Mecky Maxime, ilifunga Yanga jijini, Dar es Salaam mabao 3-0 licha ya mengine kukataliwa na mwamuzi. Uamuzi huo uliwashangaza watazamaji wengi uwanjani, hasa wale wanaoujua mchezo wa kandanda ulivyo!

Kuna wakati kulikuwa na tetesi kuwa kocha Maxime alitakiwa na Yanga naye alikuwa tayari lakini kwa masharti ya mshahara aliotaka. Ghafla akaletwa Mzungu Luc Eymael ambaye ndiye aliyeko sasa.

Ina maana Maxime alitaka mshahara mkubwa kuliko anaolipwa huyo Mzungu aliyeko Yanga sasa ambaye hupiga kelele uwanjani mwanzo mpaka mwisho wa mchezo akiwaelekeza wachezaji jinsi ya kujipanga na kucheza? Hawafundishi wakati wa mazoezi, au wachezaji hawamwelewi?

Mchezaji wa zamani wa Yanga, Mayai anasema timu hujengwa kwa miongo kadhaa badala ya msimu mmoja kama ilivyo kwa timu zetu za Tanzania! Nakubaliana na Mayai kwani timu zetu za Tanzania zimekuwa na tabia ya kusajili wachezaji wasiopungua 10 kila mwaka na kuwaacha wengi wao baada ya kipindi kifupi!

Ndo yale waliyosema wahenga kuwa: "Haraka haraka haina Baraka." Maana yake jambo linalofanywa kwa pupa huwa halitengemai au halifani. Methali hii yatufunza umuhimu wa kufanya mambo yetu kwa utaratibu ikiwa twataka yafane.

Tatizo la Simba na Yanga ni kugombea wachezaji. Kama mojawapo imeonyesha nia ya kumsajili mchezaji fulani, ingine huingia kinyemela kutaka kumsajili mchezaji yuleyule. Wachezaji hugombewa lakini baadaye huachwa na kupelekwa kwa timu zingine kwa mkopo!

Kiungo huyo alieleza kwenye makala yake kuwa timu hujengwa kwa miongo kadhaa na sio msimu mmoja kama zifanyavyo timu zetu. Anaipongeza Simba kwamba yaweza kuwa darasa kwa vilabu ambavyo kila msimu hufikiria kufanya usajili ili kuijenga upya timu ilhali kinachotakiwa ni kuendeleza ujenzi wa timu ulioanza misimu kadhaa iliyopita.

Vilevile anasema mabadiliko ya mabenchi ya ufundi ni jambo la kawaida, lakini mabadiliko yanayofanywa na vilabu vingine vya soka, hasa zinazoshiriki Ligi Kuu Bara, husababisha timu nyingi kuanza msimu kwa kujenga upya vikosi vyao badala ya kuwa na mwendelezo wa kikosi cha msimu uliopita.

Niishie hapa nisije kurushiwa mawe na mashabiki wasiojua mchezo wa kandanda ulivyo! Nawapa pole.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

## HABARI KITAIFA



Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Hosea Kashimba (kushoto), akimhudumia mwanachama wa mfuko huo, aliyetembelea maonesho ya 44 ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam kwenye uwanja wa Mwalimu Nyerere, barabara ya Kilwa jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Abuni mfumo kubaini kiwango cha taka

**Na Romana Mallya**

MWANAFUNZI wa mwaka wa tatu, Ashirafali Leveri, katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, amebuni mfumo wa kubaini kiwango cha taka na kuomba serikali, taasisi, hospitali kuutumia ili kudhibiti kuzagaa kwa taka.

Leveri ni miongoni mwa wabunifu waliokuwa kwenye Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa, maarufu Sabasaba katika chuo hicho kilichoko Kigamboni jijini Dar es Salaam, akichukua mafunzo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama).

Akizungumza na Nipashe jana, mwanafunzi huyo alisema amebuni mfumo huo kwa kutumia kifaa cha kuhifadhi taka, mfumo wake ukimjulisha mtumiaji kuwa uchafu umejaa.

"Endapo kifaa cha kuhifadhi taka kikijaa, mfumo utawasha taa nyekundu na kumpigia mhusika simu kumjulisha kuwa taka zimejaa," alisema.

Alisema ili mtu aweke taka kwenye vifaa cha kuhifadhi taka, mfumo utamtambua na kifaa husika kikifunguka chenyewe.

"Mtumiaji akitaka kujua kama taka zinakaribia au zimejaa, akiweka uchafu mfumo utamjulisha kwa kuwasha taa, ikiwaka taa ya kijani inamjulisha kuendelea kuweka, nyekundu maana yake zimejaa na ndipo mfumo utampigia simu," alifafanua.

Leveri alisema aliamua kutengeneza mfumo huo baada ya kufanya utafiti mitaani na kwenye hospitali na kubaini baadhi yao wameweka vifaa vya kuhifadhi taka lakini vimekuwa vikijaa na taka kuzagaa ovyo.

"Vifaa vya kuhifadhia taka vipo ila nimeona ni lazima kuweka mazingira kuwa safi vikijaa wahusika wapate taarifa na kuziondoa haraka badala ya kuzalisha magonjwa," alisema.

Alitoa wito kwa serikali, taasisi mbalimbali, hospitali na watu binafsi ambao watakuwa tayari kufungiwa mfumo huo, yuko tayari kufanya hivyo.

Kijana huyo aliwashauri vijana wenzake walioko vyuoni na wahitimu, wasijibweteke kwa kusubiri ajira, badala yake wabuni vitu mbalimbali ambavyo ndivyo vitakavyoacha alama katika nchi.

"Vijana tumuunge mkono Rais John Magufuli ambaye ndoto yake ni kuhakikisha nchi inakuwa na viwanda na uchumi unakua, vipaji tulivyonavyo tusivikalie, tuvifanyie kazi kwa vitendo," alisema.

Alisema ufumo huo ameubuni kwa muda wa mwezi mmoja na ametumia Sh. 150,000 kununua vifaa mbalimbali.

## Arejesha fomu ubunge Mpanda

**Na Neema Hussein,** MPANDA

ALIYEKUWA Mbunge wa Viti Maalum kwa tiketi ya Chama cha Democrasia na Maendeleo (CHADEMA), Rhoda Kunchela, amekuwa mtia nia wa kwanza kurudisha fomu ya kuomba kugombea ubunge katika jimbo la Mpanda Mjini kupitia chama hicho.

Akizungumza na wandishi wa habari, Kunchela alisema akiwa Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Katavi, hawezi kukubali kuona wanaumizwa na wanachama wenzao kwa kukisaliti chama.

Alisema chama hicho kimejengwa kwa nguvu nyingi na pia kuna watu walipoteza kazi, hivyo hawawezi kukubali kuona watu wachache wanakiharibu.

" Natoa rai kwa wagombea mwaka huu hatuko tayari kuona watu wachache wanasaliti chama. Kama kuna madiwani wamenunuliwa bora watoke kwa usalama, vinginevyo tukimjua mtu huyo tuko tayari kumchukulia hatua," alisema Kunchela.

Alisema alipokua Mbunge wa Viti Maalumu, alisimamia upotevu wa fedha katika baraza la madiwani lililopita pamoja na migogoro mbalimbali ya ardhi.

Hata hivyo, alikishukuru chama hicho kwa kumpa ushirikiano ndani ya miaka mitano alipokuwa mbunge bila ya kupata tatizo la aina yoyote.

Alisema miaka hiyo imempa ujasiri wa kuamua kutia nia ya kuingia kwenye kinyang'anyiro Cha kugombea Ubunge kwani tayari anazijua vizuri changamoto zinazowakabili wananchi.

Katibu wa chama hicho mkoa wa katavi, Almasi Ntije, alisema wamejipanga vizuri kushiriki uchaguzi pia alisema mwaka huu wanataka kuendesha siasa za kistaarabu.

# RC akoshwa mipango kujitegemea

**Na Tiganya Vincent**

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, ameipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kwa ubunifu wake katika utekelezaji wa elimu ya kujitegemea kwa vitendo uliyoiwezesha kutatua tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa katika shule mbalimbali.

Alitoa pongezi hizo jana wakati wa ziara yake ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na majengo matatu ya hospitali ya wilaya hiyo.

"Ninawapongeza sana watumishi wote na wananchi wa Kaliua kwa kuja na mpango wa elimu ya kujitegemea Kaliua ili kujenga madarasa na nyumba za walimu... hongereni kwa jitihadi ambazo zimeanza kutoa suluhisho la matatizo ya upungufu wa miundombinu shuleni," alisema.

Alisema halmashauri zilizobaki mkoani Tabora, zinatakiwa kuiga mpango huo kwa kuwa umeonekana kuleta tija na kupunguza uhaba wa madarasa na nyumba za walimu.

Akisoma taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Katibu Tawala Wilaya ya Kaliua, Simon Nyahinga, alisema halmashauri hiyo tangu mwaka 2016, iliamua kutilia mkazo elimu ya kujitegemea, ili kuboresha sekta ya elimu, afya na kilimo kwa kutumia jamii.

Nyahinga alisema kupitia mpango huo wa elimu ya kujitegemea, wamefanikiwa kuijenga jamii kuwa na utamaduni wa kujitegemea kupitia utawala bora.

Alisema kupitia falsafa ya Kaliua EK Model ya mwaka wa fedha uliopita, wamepata mafanikio makubwa ambapo jamii imeshiriki katika kufyatua na kujenga miundombinu mbalimbali ya shule.

Nyahinga alisema katika shule za msingi, jamii imefyatua matofali zaidi ya milioni 1.9 na kujenga vyumba vya madarasa 93, matundu ya vyoo 69 na nyumba 11 za walimu.

Alisema kuwa kwa upande wa sekondari, jamii imefyatua matofali zaidi ya 600,000 na kujenga vyumba vya madarasa 56 na matundu ya vyoo 36.

Katika hatua nyingine, Dk. Sengati amewapongeza watumishi na watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kwa usimamizi mzuri wa miradi ya ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

Alisema kasi wanayokwenda nayo inaridhisha na inaonyesha kuwa wamedhamiria kukamilisha majengo hayo kwa wakati, ili wananchi waanze kupata huduma.

# Ujenzi barabara mzunguko Dodoma waiva

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetia saini mikataba ya ujenzi wa mradi wa barabara za mzunguko katika jiji la Dodoma kwa kiwango cha lami, zenye urefu wa kilomita 112.3 utakaogharimu Sh. bilioni 494.

Fedha kwa ajili ya ujenzi huo ni mkopo wenye riba nafuu kutoka Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB).

Hafla ya utiaji saini ujenzi wa barabara hizo ilifanyika jana jijini hapa ukishuhudiwa na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe pamoja na manaibu wake wawili.

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri Kamwelwe alisema mradi huo utajengwa na makandarasi wawili ambao ni CCECC pamoja na Avic International, kampuni zote kutoka nchini China.

Alisema ujenzi wa mradi huo utakuwa sehemu ya mtandao wa barabara za jiji la Dodoma ambao utasaidia kuunganisha mikoa na nchi za jirani.

"Ujenzi wa mradi huu kwanza utatoa fursa ya ajira kwa wananchi lakini wito wangu ni kuhahakikishia makandarasi wanamaliza kazi yao katika muda uliowekwa kwa mujibu wa mkataba" alisema Kamwelwe.

Pia alisema serikali tayari imeshatenga fedha kwa jili ya kulipa fidia, ambayo itatolewa kwa mujibu wa sheria kwa kufuata utaratibu na si vikundi vya mitaani.

"Watu wamekuwa wakinifuata ofisini kwangu na kujitambulisha wao ndio wawakilishi wa kamati za ufuatiliaji fidia nimewafukuza. Mkuu wa wilaya hayupo mimi nitazungumzaje na wewe kuhusu fidia hata zikujui," alisema Kamwelwe.

Awali, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (Tanroads), Mhandisi Patrick Mfugale, akitoa maelezo kuhusu mradi huo, alisema fedha za utekelezaji wa ujenzi huo ni kutoka AfDB na kiasi kingine ni kutoka serikalini.

"Fedha ya ujenzi wa mradi huu ni mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika Sh. bilioni 412 na serikali itachangia Sh. bilioni 82, sawa na asilimia 16.5 ya kiasi chote cha fedha," alisema Mfugale.

Alisema awamu ya kwanza ya mradi huo itajengwa na mkandarasi CCECC ambaye atajenga barabara yenye urefu kwa kilomita 52.3 kwa gharama ya Sh. bilioni 100.84.

Awamu ya pili, alisema itajengwa na Avic International ambaye atajenga barabara yenye urefu wa kilomita 60 kwa gharama ya Sh. bilioni 120.86 bila kodi ya ongezeko la thamani (VAT).

"Kipande cha kwanza cha urefu wa kilomita 52.3, mkandarasi atajenga kwa muda wa miezi 39 na kile cha pili chenye urefu wa kilomita 60 kitajengwa kwa miezi 42," alibainisha Mfugale.



Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), Mhandisi, Patrick Mfugale (kulia), akibadilishana mkataba na Mkurungenzi Mtendaji wa kampuni ya ujenzi ya kichina ya CCECC, Zhang Jun Le, baada ya kusaini mkataba wa ujenzi wa barabara za mzunguko za jiji la Dodoma, zenye urefu wa km 52 kwa thamani ya Sh. bilioni 100.8 jijini humo jana, na kushuhudiwa na Waziri wa Ujenzi Isack Kamwelwe na mainabu wawili wa wizara hiyo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Uwezo, uchumi chanzo kunyanyasika wanawake

**Na Julieth Mkireri**

MKURUGENZI Mtendaji wa taasisi ya kisheria ya huduma muhimu za kijamii ya ESS Creative and Legal Foundation, Erick Mukiza, amesema kukosekana kwa uelewa kuhusu msimamizi wa mirathi ni chanzo cha baadhi ya wanawake kunyanyasika na kupoteza haki zao.

Mukiza alibainisha hayo juzi kuwa kukosekana kwa elimu sahihi ya mirathi kumekuwa pigo kwa kundi hilo ambalo linaonekana kukosa sehemu ya kupata haki zao na kuacha mali za urithi kwa watu ambao si wahusika.

Alisema kundi la wanawake lipo kwa wananchi wa kati ambao wamekosa msaada wa kisheria kutokana na kipato chao, hivyo kupoteza haki zao na wengine kudumu kwenye manyanyaso kwa muda mrefu,

Kutokana na ombwe hilo, alisema taasisi yake iliyoanzishwa miaka saba iliyopita, imeanza kutoa huduma kwa kundi hilo ambalo limekuwa likihangaika na kukosa haki kwa kushindwa kulipa gharama za wanasheria.

"Awali tulikuwa tunatoa huduma za kisheria za kawaida kwenye vikundi vya wajasiriamali ambao wengi walikuwa kwenye mikopo na kupoteza vitu vyao baada ya kushindwa kurejesha. Tumefanya pia na maeneo mbalimbali lakini tuliokuwa tukiwahudumia wengi hawana uwezo wa kulipa gharama zinazotakiwa.

Hawa ni wale ambao baadhi yao katika kundi hili kipato chao ni kidogo, hivyo kulipa gharama za sheria kwao inakuwa changamoto tukaona tuanze utaratibu wa kuwasaidia kwa gharama nafuu. Watalazimika kuwa wanachama kwa kununua kadi zitakazowawezesha kuchanga kila mwezi," alisema Mukiza.

Alisema katika taasisi hiyo kuna kadi za aina nne ambazo mwanachama akijiunga atakuwa akichangia kila mwezi na mchango ambao unaanzia Sh. 30,000.

Mkurugenzi huyo alisema baada ya kuanzisha utaratibu huo mwaka 2018, wamekuwa wakipokea zaidi kesi za ndoa, ardhi, mirathi na ajira ambazo wanawake wananyanyasika.

Alisema katika kesi hizo kundi la wanawake ndio wanaonyanyasika na wanaume ambao wana fedha na wana uwezo wa kuwalipa wanasheria kuendesha kesi zao.

"Wanawake wamekuwa wakinyanyasika zaidi. Wanaume wao wanajiaminisha kwa kuwa wana fedha za kulipa mawakili na hawa wanawake hawana uwezo, hivyo wanakosa haki zao kwenye ndoa na hata mirathi," alisema.

# Shule yajivunia kutoa viongozi

**Na Stevie Chindiye,**

**MBINGA**

SHULE ya Sekondari ya Kigonsera iliyoko wilayani Mbinga mkoani Ruvuma, imetamba kuweka historia ya kipekee hapa kwa kutoa viongozi wawili wa ngazi ya juu kabisa nchini.

Mkuu wa Shule hiyo, Ponsiano Ndunguru, alibainisha hayo juzi kuwa shule hiyo ilianzishwa mwaka 1938 ikiwa seminari ya Kanisa Katoliki chini ya Shirika la Wabenedikitini wa Peramiho na mwaka 1961 kuchukuliwa na serikali, ina historia ya kuweka rekodi hiyo.

Katika taarifa hiyo, Ndunguru aliwataja viongozi hao kuwa ni Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa ambaye alisoma toka mwaka 1952 hadi 1953 kisha alihamia Ndanda mkoani Mtwara na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa ambaye alianza kidato cha kwanza na kuhitimu kidato cha nne mwaka 1980.

Licha ya viongozi hao, alisema shule pia imetoa viongozi wengine wengi wakiwamo aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Usalama wa Taifa na Balozi wa Tanzania nchini Msumbiji, Dk. Modestus Kipilimba na Prof. Simon Mbilinyi aliyewahi kuwa Waziri wa Fedha na Mbunge wa Peramiho.

Aliwataja wengine kuwa ni Juma Homera ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Katibu Mkuu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Frolens Turuka, Askofu Mstaafu wa Jimbo la Mbinga, Emmanuel Mapunda, Askofu Mstaafu wa Jimbo la Njombe, Raymund Mwanyika (wote ni marehemu) Askofu Mkuu Mstaafu wa Jimbo Kuu la Songea Norbert Mtega na Askofu wa Jimbo la Lindi, Bruno Ngonyani.

Katika kundi hilo pia wamo Askofu wa Jimbo la Mtwara, Gabriel Mmole na Askofu wa Jimbo la Njombe, Alfred Maluma.





Mwenyekiti wa Baraza la Maaskofu wa makanisa ya Kipentekoste Tanzania (CPCT), Askofu Peter Konki (wa pili kushoto), akisoma tamko la kumpongeza Rais Dk. John Magufuli, kwa kuona umuhimu wa kumtegemea Mungu, katika uendeshaji na usimamizi wa nchi, lililotolewa na maaskofu hao, jijini Dodoma jana. Wengine ni Mjumbe wa kamati tendaji, Askofu Deo Lubala (kulia), Makamu Mwenyekiti Baraza hilo, Askofu Sheggha Bath-

# Ma-RC wapewa jukumu kuubadili sura Ushirika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KUTOKANA na shughuli za Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuhamishiwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), wakuu wa mikoa nchini wamegizwa kujipanga kubadili sura ya ushirika nchini.

Agizo hilo lilitolewa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Selemani Jafo, alipofungua kikao kazi kati yake na wakuu hao kujadili masuala mbalimbali ya ushirika.

Alisema serikali imeamua kuhamishia shughuli hizo TAMISEMI kwa asilimia 100, ili kuleta ufanisi katika ushirika, hivyo wakuu hao wanatakiwa kufahamu idadi au vyama vya ushirika vilivyoko kwenye maeneo yao.

"Mhakikishe mnafahamu udhaifu ulioko ndani ya vyama hivyo na kuhakikisha mnaweka mikakati itakayofanya ushirika uwe na sura tofauti na ushirika wa sasa.

"Siku zote lengo la mabadiliko yoyote ni kuleta ufanisi, hivyo ni imani yangu kwa usimamizi wa wakuu wa mikoa utakuwa na mabadiliko makubwa ya ufanisi uonekane uko tofauti, na kujibu changamoto ambazo zinaukabili ushirika kwa sasa," alisema.

Jafo alisema hatua ya kuhamisha Tume ya Ushirika kwenda TAMISEMI imechukuliwa baada ya kubainika kuwapo upungufu mwingi wa kimuundo kwa sasa.

"Katika kutimiza wajibu wake wa kuwahudumia wananchi, kupeleka uchumi mbele katika maeneo mbalimbali ambayo tume hii imekuwa ikifanya kazi yake ndiyo yamekuja mabadiliko haya na ina maana kuwa wakuu wa mikoa ndiyo wasimamizi wakubwa wa ushirika katika mikoa yao," alisema.

Alisema kutokana na muundo wa sasa, ilikuwa ni vigumu kwa mkuu wa mkoa kuingilia kati ushirika inapobainika kuwapo dosari na hata warajis wa mikoa walikuwa hawajibika ipasavyo kwa wakuu wa mikoa.

"Tume hii sasa inafanya majukumu yake chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ni vyema wakuu wa mkoa wawe na nguvu ya kisheria ya kusimamia ushirika katika mikoa yao. Mkuu wa mkoa aone atafanya nini kwa lengo kuwahudumia wananchi waliojiunga katika ushirika,"aliagiza.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Joseph Nyamhanga, alisema wakuu hao watajengwa uwezo katika sheria ya ushirika na utendaji wa vyama vya ushirika pamoja na masuala ya kuzingatia katika uendeshaji vyama vya ushirika.

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, alipongeza uamuzi huo wa serikali na kusisitiza kwa nguvu ya kisheria waliyopata, watahakikisha wanasimamia ushirika kwa karibu na kutoa onyo kwa wabadhirifu wa ushirika.

# Uwiano huduma za afya sasa waridhisha

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imefanikiwa kuhakikisha kunakuwa uwiano wa kutosha katika utoaji huduma za afya na wananchi kupata huduma za afya za uhakika na wakati.

Hayo yalisemwa jana na Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa Abel Makubi, alipofungua kikao kati ya Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kujadili utoaji huduma bora za afya kwenye vituo vya afya, hospitali za halmashauri na rufani zilizojengwa na kukarabatiwa na serikali.

Alisema wataalamu wana wajibu wa kuendeleza chachu ya maendeleo yaliyofikiwa na kuhakikisha vituo hivyo vinafunguliwa kwa kuzingatia utaratibu unaotakiwa na kuendelea kutoa huduma vikiwa na vifaa vyote muhimu na wataalamu wenye weledi na stadi katika kupambana na magonjwa na kupunguza vifo vinavyozuilika.

Profesa Makubi alibainisha kuwa mafanikio hayo yamepatikana kutokana na sekta ya afya kuchukua jukumu la kufanya ukarabati wa ujenzi katika vituo vya kutolea huduma za afya ambapo iliweka kipaumbele kwenye vituo vya afya vya msingi, ili kuviwezesha kutoa huduma za dharura za uzazi na mtoto mchanga.

"Tumejenga hospitali mpya za wilaya 99 kutoka hospitali 70 za awamu ya kwanza zimekamilika na nyingi zimeanza kutoa huduma. Hata hivyo, serikali imeongeza kujenga hospitali nyingine 29 na fedha zake zimetengwa tayari," alisema.

Awali, Mkurugenzi wa Huduma za Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii, TAMISEMI, Dk. Ntuli Kapologwe, alisema kikao hicho kina lengo la kuwa na mwelekeo mzuri wa sekta ya afya, hivyo ushirikiano wa pamoja kati ya wizara hizo mbili ni muhimu katika kufanikisha na kusukuma mbele sekta hiyo nchini.

Mkurugenzi wa Huduma za Kinga kutoka Wizara ya Afya, Dk. Leonard Subi, alisema vituo vya afya 570 vilivyojengwa na kukarabatiwa na serikali, vimeboresha huduma za afya na kuzuia vifo vya kinamama wajawazito na watoto wachanga huku vikiwa na uwezo wa kutoa huduma za dharura kama upasuaji.

## Wadau mkonge kumpa tuzo JPM

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WADAU wa zao la mkonge, wanatarajia kumpa tuzo Rais John Magufuli kwa kuinua zao hilo nchini kabla ya kumaliza kipindi chake cha pili cha uongozi.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Rehema Nchimbi, katika kikao cha wadau wa zao hilo kilichofanyika jijini hapa jana, aligusia nia ya kutolewa kwa tuzo hiyo.

Alisema kwa kipindi kifupi cha utawala wake, Rais Magufuli amefanya jitihada za kuinua zao hilo.

Mkuu huyo alisema kuwa zao hilo miaka ya nyuma ndiyo lilikuwa linaongoza kwa kuliongezea taifa mapato, hivyo watahakikisha wanatumia mbinu zilezile kulirudisha zao hilo kwenye ubora wake. "Kipindi cha nyuma zao la mkonge lilikuwa linaongoza kwa kuliongezea mapato taifa kwa asilimia 65, hivyo mkakati uliopo sasa ni kulirudisha zao hilo na kushika nafasi ya kwanza katika uzalishaji nchini," alisema. Nchimbi alisema kuwa, katika utawala wa Rais Magufuli, mambo ambayo yalidhaniwa hayawezekani, yamewezekana.

"Unajua hapa Dodoma ndiyo madhabahu ya Rais Magufuli ambaye alimwomba Mungu yakafanyika mambo makubwa katika muda mfupi, sasa na sisi tutumie madhabahu hiyo hiyo kufufua za la mkonge,"alisema Nchimbi.


Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Mkonge, Saad Kambona, alisema kuwa wameweka mkakati ya kuinua zao hilo kwa kuwashawishi wakulima wadogo kulima zao hilo ili uzalishaji uongezeke kwa kasi.

"Unajua baadhi ya watu wanafikiri kilimo cha mkonge kinafanywa na wakulima wakubwa tu, siyo kweli, hata wakulima wadogo wadogo wakifanya kilimo hicho kwa wingi, uzalishaji utakuwa mkubwa na serikali itaongeza pato la taifa," alisema Kambona. Mkurugenzi huyo alisema kuwa hivi sasa, wanazalisha tani 36,000 ambapo mkakati uliopo ni kuzalisha tani 120,000 hadi 150,000 kwa mwaka.

Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, alisema serikali ina mpango wa kuinua zao hilo nchini, ili kuhakikisha linafikia malengo waliojiwekea.

Alisema serikali haitakuwa tayari kuona waliopewa viwanda wanaviatamia badala ya kuviendeleza ili kuwasaidia wakulima wa mkonge nchini.

"Serikali haitakuwa tayari kuwavumilia wenye viwanda ambavyo hawavifanyii kazi, tayari nimemwagiza Msajili Hazina aanze kuwasaka wanaoatamia viwanda," alisema Mgumba.





Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wahamaji (IOM), Dk. Qasim Sufi (kushoto), akikabidhi msaada wa pikipiki kwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Halima Maulid Salum katika hafla iliyofanyika katika wizara hiyo, eneo la Mnazi Mmoja, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Watoa pikipiki kusaidia wafanyakazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar, imepokea msaada wa pikipiki mbili zenye thamani ya Dola 2,727 (Sh. milioni 6.319) kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wahamaji (IOM), ili kuwasaidia wafanyakazi kufuatilia maradhi ya corona.

Akikabidhi msaada huo jana, Mkuu wa Shirika la Wahamaji Tanzania Dk. Qasim Sufi, huko Wizara ya Afya Mnazimmoja, alisema lengo la msaada huo ni kuiwezesha na kuirahisishia Serikali ya Zanzibar katika jitihada za kupambana na maradhi hayo.

Alisema shirika hilo litazidi kutoa ushirikiano katika sekta ya afya, ili kupambana na maradhi mbalimbali ikiwamo ya kuambukiza.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Halima Maulid Salum, alisema pikipiki hizo zitawawezesha kufuatilia mwenendo mzima wa maradhi. Alisema pikipiki hizo zitawasaidia katika kufanya utafiti wa maradhi mbalimbali hasa maeneo ya ndani ambayo ni vigumu kufikika kwa kutumia usafiri wa gari.

"Baadhi ya sehemu hasa vijijini inakuwa usumbufu kufika kwa gari, hivyo msaada huu utatusaidia kwa kiasi kikubwa," alisema Naibu Katibu Mkuu huyo.

Mkurugenzi wa Kinga, Dk. Fadhil Mohamed, alilishukuru shirika hilo kwa msaada huo na kuwataka wafanyakazi kuzitumia vizuri pikipiki hizo ili kufikia malengo. Aliwataka watendaji waliokabidhiwa pikipiki hizo kuzitumia ipasavyo na kuzitunza ili zidumu.

# Aonya wanaodai kupewa jukumu maalum mitaani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Kaskazini Unguja, Rajab Ali Rajab, amewataka masheha katika wilaya hiyo kuwa makini na watu wanaojitokeza katika shehia zao kwa visingizio vya kuwa wameagizwa na serikali kufanya kazi maalum kabla ya kupata taarifa sahihi kutoka ofisi ya wilaya.

Alisema katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu kuna baadhi ya watu wamekuwa wakijitokeza katika shehia kwa visingizio vya kufanya utafiti wa mambo mbalimbali ikiwamo suala la ulinzi na usalama, jambo ambalo linaweza kuhatarisha amani na utulivu uliopo katika maeneo hayo.

Akizungumza na masheha ofisini kwake Mahonda jana, Mkuu wa Wilaya huyo alisema kisheria sheha ni mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama katika shehia yake hivyo ni vyema kwa kipindi hiki kuwa mstari wa mbele kuhakikisha wanatoa taarifa kwa uongozi wa wilaya, ili wachukuliwe hatua kabla ya kuathiri jamii.

Alisema suala la amani na utulivu ni muhimu kwa wananchi, hivyo ofisi yake haitakuwa tayari kuona baadhi ya watu wanarudisha nyuma juhudi hizo kwa kuingia katika wilaya na kufanya utafiti bila kufuata taratibu za kiserikali.

Ofisa Vijana wa Wilaya hiyo, Mboja Ussi Kali, aliwataka masheha hao kuhamasisha vijana katika shehia zao kujitokeza kwa wingi kuchukua fomu za kujiunga na mafunzo ya amali ambayo yanatarajiwa kutolewa na Wizara ya Vijana, Wazee, Wanawake na Watoto bila ya malipo yoyote, ili kila kijana anufaike na fursa hiyo.

Alisema kuwa serikali kwa kupitia wizara hiyo, imeandaa mkakati maalum wa kutoa elimu ya ujasiriamali kwa vijana hao hasa kwa wanawake pamoja na watu wenye uhitaji maalum, ili kuondoa tatizo la ajira nchini.

# Utumiaji vyandarua uko chini asilimia 59

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

UTUMIAJI wa vyandarua Zanzibar upo chini kwa asilimia 59, hali inayochangia kuongezeka kwa maradhi ya malaria.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Ofisa Tathmini wa Ufuatiliaji Kitengo cha Kumaliza Malaria Zanzibar, Mohammed Haji Ali, alisema watu 8,869 wameugua ugonjwa wa malaria visiwani Zanzibar kuanzia Januari hadi Juni, mwaka huu.

Alisema kati ya wagonjwa hao, 5,500 waliripotiwa kuanzia Januari hadi Machi na wengine 3,369 waliripotiwa kuanzia Aprili hadi Juni.

Alisema kuwa Oktoba hadi Desemba mwaka jana, Zanzibar iliripoti wagonjwa wa malaria 3,635.

Ofisa huyo alisema ongezeko la wagonjwa hao limesababishwa na kuwapo mazalia mengi ya mbu yaliyochangiwa na mvua ya masika iliyomalizika hivi karibuni.

Alisema endapo wananchi watatumia vyandarua kwa usahihi, ugonjwa huo utaondoka kabisa.

Alisema kitengo hicho tayari kimeanza kuchukua hatua za tahadhari kwa kuwakinga wananchi ikiwamo kupanga mikakati ya kunusuru jamii kuambukizwa zaidi.

Alitaja mikakati hiyo kuwa ni pamoja na kuelimisha jamii kujilinda na ugonjwa huo, kuwapima wananchi ambao katika maeneo yao kuna maambukizi mengi, kugawa vyandarua kwa wananchi wote katika shehia na kampeni ya kuelimisha jamii kuhusu matumizi ya kinga ya malaria.

Aliitaja mikakati mingine kuwa ni pamoja na kufuatilia wagonjwa wa malaria majumbani baada ya kupata ripoti kutoka hospitali na vituo vya afya.

Ofisa huyo alitoa wito kwa wananchi kubadilika kwa kutumia vyandarua kujikinga na malaria kwa sababu ugonjwa huo bado upo.



ROSE REE
UKURASA 12

Nipashe BT
JUMAMOSI JULAI 11, 2020



## HATA SHETANI ANASHANGAA

# Shilole ilikuwaje shubiri akaona asali?

WAPO wanaosema ni ndoa ya laana, wengine walifika mbali kwa kuita ni ndoa ya kikatili ambayo hata shetani mwenyewe akisikia anasikitika.

Mazingira hayo magumu ndiyo yalikuwa yakitawala katika maisha ya ndoa kati ya mwanamuziki na mjasiriamali, Shilole na mumewe Ashraf Sadiki, maarufu kama Uchebe.

Kwa mazingira ya nje wanandoa hao walikuwa wakiishi kwa furaha na mapenzi motomoto, lakini ndani ya pazia kulitawala ukatili wa hali ya juu, kiasi ambacho unaweza kusema ilikuwa 'ndoa ya laana' ambayo binadamu mwenye roho nyepesi asingeweza kudumu hata kwa siku mbili.

Wiki hii, Shilole, aliamua kuvunja ukimya kwa kutoa ujumbe mzito unaoelezea ushetani huo ambao kwa nje haukuonekana, badala yake ilionekana kama wanandoa hao walikuwa na mashamsham ya mahaba niue na upendo.

Baada ya ujumbe huo mzito, watu mbalimbali walitoa maoni yao wakiwamo viongozi wa kisiasa, wasanii na wanaharakati, wote walifikia ukomo wa kusema ni kitendo cha kishamba kwa mwanamume kumpiga mkewe kama gunia la chumvi, eti kwa sababu amemkosea.

Kwa mfano, mwanasheria maarufu, Albart Msando, aliandika maneno mazito akimshangaa Uchebe kuuvaa ushetani huo, huku akijitetea matukio yote alifanya zamani.

Msando alimalizia kwa kusema "Nitashangaa kama 'upelelezi bado unaendelea' mpaka ikifika mwezi wa nane. Ni vyema muda akitoka jela akute kiberiti kinauzwa elfu 15 na box spanner inauzwa kama laki 6 hivi. Tuone gereji atakuwa na spana ngapi na ghetto atawasha jiko la mchina ,"

Hitimisho la mwanasheria huyo, linaweka wazi kwamba hata shetani mwenyewe atashangaa kama suala hilo litaishia hewani, kwani hata yeye pamoja na kuitwa majina mabaya na kupewa laana zote, kwa hili amepigwa na butwaa.

Jambo la kushangaza na kujiuliza ilikuwaje Shilole, akavumilia na kuona maumivu yote hayo sawa na asali hadi sasa ndipo akaamua kusema machungu yake?

Pamoja na watu kuendelea kupambana kwenye mitandao kueleza hisia zao, mwisho watasikitika tu, lakini wawili hao ndio wataweza kuamua kama kweli yametimia, au wanataka kuleta sehemu ya pili ya ndoa hiyo yenye mashaka.

BASI SAWA

## Ndoa yanukia Billnas, Nandy

HARUSI inanukia! Ndivyo inaelekea kwa wasanii wawili mastaa, Nandy na Billnas, kuwa katika harakati za mwisho kufikia hatua ya kufunga ndoa rasmi.

Katika kiashiria cha wawili hao kunusa maisha ya mke na mume, hivi karibuni Billnas alipelekwa ukweni kwa Nandy kuko Usangi,wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro.

Kupitia picha ambazo wameposti katika kurasa zao za mtandao wa kijamii wa Instagram inaonyesha kuwa Nandy amempeleka Billnass katika familia yake kwa kumkutanisha na Baba, Babu na bibi yake.

"Niko na mwenye jina lake Nandera, bibi yangu kipenzi na babu yangu kipenzi upareni kwetu, tuko na baba mzaa vyema na watoto wake Charles Mfinanga" ameandika Nandy



## 'Killer Boy' kutoka kucheza disko hadi kumiliki bendi

YAWEZEKANA jina la Killer Boy likawa geni kwa baadhi ya watu, lakini wadau wa disko na muziki wa dansi watakuwa wanalijua vizuri, kwani jina hilo linaendelea kuvuma kivingine.

Bingwa huyo wa zamani wa kucheza disko wa mkoa wa Morogoro, sasa amekuwa mkurugenzi wa bendi ya muziki wa dansi ya Waluguru Original yenye maskani yake mjini humo.

Killer Boy anamiliki bendi hiyo yenye wanamuziki 14 na waneguaji wa nne.





## Rose Ree wanaume wote si makatili

RAPA wa kike anayefanya vizuri kwenye Bongo Fleva, Rosa Ree, amefananisha tukio la kupigwa kwa Shilole, sawa na mama yake mzazi alivyonyanyaswa na baba yake.

Akizungumza na EATV, Rosa Ree amesema suala la mama yake kufanyiwa ukatili mbele yake linamuathiri kwenye maisha yake hadi kwa ndugu zake.

"Niliona tukio lile Instagram kiukweli limenisikitisha sana, nimepata uzoefu wa kuona ukatili kwenye uhusiano japo haukuwa wangu, ila ni kwa wazazi wangu, najua inavyokuwa kwa mwanamke kupitia kitu kama kile, nilikuwa namtizama mama yangu ni kitu ambacho kimeathiri maisha yangu " amesema.

## Mchawi ni ndugu yako

**Na Adam Fungamwango**

KIKULACHO ki nguoni mwako. Ni msemo wa kiswahili unaofasirika kwamba kinachokutafuna kipo karibu yako.

Hii ina maana kwamba mtu yoyoye anayekufanyia ubaya, basi ni lazima anakufahamu vizuri. Adui yoyote anayetaka kushinda vita kirahisi ni lazima kwanza ajue udhaifu wako ndipo atakapoandaa silaha zinazotosha kukumaliza.

Filamu ya kusikitisha iitwayo 'Sikitu' imeonyesha kila kitu kinachohusiana na hicho.

Imechezwa na Kajala Masanja, Hemed Suleiman, Taira Odera, Matra Taimamu, hayati mzee Majuto, Tausi Mgendela, Asha Boko na wengineo wengi.

Hemed na Kajala ambaye amecheza kama Sikitu ni mke na mume. Ni watu wenye uwezo na wanaishi maisha ya kifahari.

Sikitu anapatwa na ugonjwa unaomfanya ashindwe kufanya chochote kile. Hemed anaamua kumrudisha nyumbani kwao kwa ajili ya matibabu, pia kupata muda wa kupumzika.

Hata hivyo, Hemed anaingia kwenye penzi na mdogo wa mkewe, Taira. Penzi hilo linakuwa moto moto hadi inakuwa si siri tena. Wazazi pia wanafahamu hilo. Kuwakanya ilikuwa ni kazi bure.

Mwenyewe Sikitu anagundua hilo. Hali yake inazidi kuwa mbaya, anapatwa na mshtuko wa moyo unaosababisha kupooza mwili. Hatimaye anakata roho.

Hemed na Taira wanakwenda msibani, lakini mzee Majuto ambaye ni baba wa mabinti wote wawili, Sikitu na Taira, anamtimua Hemed na mpenzi wake Taira kwa madai wao ndiyo wamesababisha kifo cha binti yake.

Siku isiyo na jina, majambazi wanavamia nyumbani kwa Hemed. Wanataka wamuonyeshe alipoweka hazina ya pesa. Wakati mwenyewe Hemed akisuasua, Taira aliwaonyesha majambazi mkoba wa pesa ulipo.

Kwa mastaajabu, majambazi baada ya kuchukua mkoba ule, wanamkabidhi mmoja wa watu ambao wamewaweka chini ya ulinzi, si mwingine ni Taira.

Ananyanyuka na kuchukua mkoba wa pesa, akamgeukia Hemed na kumwambia hakuwa na mapenzi ya kweli, badala yake alikuwa anazitaka zile pesa tu. Bastola aliyokuwa nayo mkononi ilitosha kumtoa uhai Hemed. Wakati wale majambazi wakidhani watalipwa ujira wao kwa kazi ile, nao wanauawa.

Tayari Taira akajiona mshindi, kumbe mdogo wa Hemed, Matra alikuwa amefika nyumbani hapo na kushuhudia mchezo mzima.

Wakati Taira anatoka, Matra alinyanyua kistuli na kumpiga nacho kichwani, akapoteza maisha hapo hapo. Mkoba wa pesa ukawa mikononi mwa Matra, mdogo wa Hemed ambazo alizipeleka kwa wazazi wake.





## Jitu Baya awarusha mikono 'Yaani Oohhh'

MWANAMUZIKI wa kufokafoka anayekuja kwa kasi, Jitu Baya, ametambulisha ngoma yake mpya inayokwenda kwa jina la 'Yaani Oohh'.

Jitu baya akizunguma na BT, amesema wimbo huo ambao umerekodiwa kwa Ammy Waves, umeanza kuruka hewani wiki hii na unalenga kuwapa raha mashabiki wake.

Msanii huyo wa rapa ambaye sauti yake inafananishwa na mkongwe Chidi Benz, anatamba na kibao chake cha 'Flow Kali' amesema wimbo huo ni maalum baada ya kupungua kwa ugonjwa wa corona.

"Baada ya kupungua kwa corona na serikali kufungua vikwazo ili maisha yaendelee, nimeamua kuwarusha mashabiki wangu kwa wimbo huo ambao utawafanya kupata furaha zaidi," amesema Jitu Baya.




## Tano zilizonoga za Dede

**Na Adam Fungamwango**

NI miaka mitatu sasa imepita tangu alipofariki mmoja wa wanamuziki bora kabisa nchini Tanzania, Shaaban Dede Kamchape.

Ilikuwa ni Julai 7, 2017 kwenye Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Tanzania ilipompoteza mwimbaji wa sauti ya kwanza, tamu kama kinanda, lakini pia mtunzi wa mashairi murua, alipokuwa amelazwa akitibiwa matatizo ya ugonjwa wa kisukari.

Dede alifariki akiwa na umri wa miaka 58, akiwa ameacha jina kubwa nchini kwenye tasnia ya muziki kwenye bendi mbalimbali alizopita.

Julai 7, mwaka huu, alitimiza miaka mitatu akiwa chini ya tumbo la ardhi, akiwa amelala kwenye makaburi ya Kisutu jijini Dar es Salaam.

Mwanamuziki huyo alizaliwa Kanyigo mkoani Kagera mwaka 1959 na alipigia bendi mbalimbali kama Tabora Jazz, Dodoma International, Juwata Jazz, DDC Mlimani Park Orchestra, Bima Lee, na Orchestra Safari Sound (OSS).

Bendi ya Juwata alipigia mara tatu na Mlimani Park mara mbili. Leo tutatazama baadhi ya nyimbo zake tano bora kabisa ambazo alizitunga na kuziimba kwa ustadi wa hali ya juu, akiwa na bendi mbalimbali nchini.

**Maisha ni Vita (Juwata Jazz)**

Huu ndiyo wimbo ambao ulimtambulisha rasmi kwenye bendi ya Msondo Ngoma alipojiunga mwishoni mwa miaka ya 70, baada ya Hassan Bitchuka kuondoka kwenye bendi hiyo na kwenda DDC Mlimani Park Orchestra.

Ni wimbo ambao maudhui yake ni kwamba mwanamume anamuaga mkewe Fatuma kuwa anakwenda safari ya kikazi, huku akimwambia amuombee dua afike salama. Anamuasa atunze watoto, ajichunge na yeye pia, kwani maisha ni vita, mtu analala mbali na familia yake kwa ajili ya pesa tu.

**Talaka Rejea (DDC Mlimani Park)**

Dede alihama Msondo na kwenda Sikinde mwanzoni mwa miaka ya '80, na kutunga wimbo uliotokea kuwa maarufu sana nchini 'Talaka Rejea'.

Maudhui yake ni mwanamama akimtuhumu aliyekuwa mumewe kuwa alimtaliki kwa talaka rejea na kumnyang'anya nguo mbele za watu. Lakini cha ajabu leo anataka kurudiana naye.

Mwanamama kwa upande wake hataki tena kwa mabaya yote aliyotendewa.

**Shangwe na Harusi (Bima Lee)**

Mwaka 1984, Dede alihama Sikinde na kwenda Bila Lee akiasisi mtindo na 'Magnet Tingisha'.

Huko alitunga na kuimba kibao kilichopendwa mno kiitwacho 'Shangwe ya Harusi'.

Katika kibao hicho ni kwamba jamaa analalamika kukimbiwa na bi harusi.

Akiwa kwenye sherehe za kufunga ndoa, anaingia kwenye chumba cha bi harusi, lakini hamkuti.

Kutoroka kwa bi harusi kunamfanya jamaa kulalamika kweli kweli.

**Kimwaga (Juwata Jazz)**

Alirejea tena Msondo katikati ya mwaka '80 kuelekea mwishoni na kutunga vibao kadhaa, lakini kilichokuwa maarufu zaidi ni 'Kimwaga.'

Jamaa anamtuhumu mpenzi wake kuwa anamtangazia kwa watu kuwa anahonga sana. Kutokana na hilo, jamaa anamwambia anampa pesa kwa sababu siyo bwege, bali ni mapenzi, japo penzi ni maelewano, lakini mkono mtupu haulambwi, hivyo aache kumsemasema vibaya.

**Nyumba na Mgumba (OSS)**

Mwishoni kabisa mwa miaka ya '80, Dede alielekea Orchestra Safari Sound (OSS), huko nako kama kawaida, alitunga vibao vingi, lakini kilichopendwa na wengi ni 'Nyumba ya Mgumba Haina Matanga.'

Ni wimbo ambao jamaa analalamika kutokuwa na mtoto. Anasema amejaaliwa elimu, ilimpatia heshima na ana uwezo wa kununua chochote duniani, lakini ugumba umevunja heshima yake.





# D'banj azidi kutetewa ubakaji

MENEJA wa zamani wa mwanamuziki maarufu Nigeria, D'banj, ameingilia sakata la ubakaji linalomkabili msanii huyo, akisema tuhuma hizo si za kweli na kudai mlalamikaji alilipwa pesa kuibua tuhuma hizo.

Franklyn Amudo, ambaye alikuwa meneja wake D'banj, amesema Seyitan Babatayo, ambaye anadai rafiki wake wa kike alibakwa na mwanamuziki huyo alilipwa kiasi cha dola 100 katika hoteli moja kwa ajili ya kutengeneza tuhuma hizo.

Amudo alisema hayo katika kipindi cha maswali kwenye kituo kimoja cha televisheni, kwamba hata chumba ambacho kinadaiwa D'banj alifanya unyama huo hakijui na kwamba amesingiziwa.



## Ini Edo ukiwakumbuka wanawake wenzio utafaulu

MWIGIZAJI mkongwe wa Nollywood, Ini Edo, ameanzisha mpango wake wa kuwainua wanawake vijana wa Afrika kwa kutumia teknolojia.

Msanii huyo wa kike ambaye amejikusanyia wafuasi wengi, amesema ameamua kuanzisha mpango huo kwa ajili ya kuwasaidia wanawake katika ujasiriamali na ushauri wa kiuchumi.


Amesema katika kukamilisha mkakati huo ataandaa jopo la uteuzi wa washiriki na kwa kuanzia itakuwa katika mji aliozaliwa.

## Kanye West, wewe na 'White House' wapi na wapi

RAPA staa wa Marekani, Kanye West, amesisitiza kuwa nia yake ya kuwania urais itabaki palepale.

Katika ujumbe wake wa Twitter, mwanamuziki huyo amesema ni lazima atatekeleza ndoto yake ya kuingia chumba cha 'Oval Office' katika Ikulu ya White house ambacho kinatumiwa na kiongozi wa nchi hiyo yenye nguvu Duniani.

"Nataka kuwaambia ahadi yangu kwa Marekani na kuamini Mungu, kwamba nitatekeleza maono yangu na kujenga ya baadae kwa kuwania Urais wa Marekani," ameandika West.





## Davido, Chioma mambo murua

BAADA ya kuenea kwa uvumi kwamba mwanamuziki nyota, Davido, amebwagana na mchumba wake Chioma, sasa mambo yanaonekana kuwa shwari baada ya kuwekwa mtandaoni video fupi ikiwaonyesha wawili hao wakiwa na furaha.

Chioma Rowland ambaye ni mama wa mtoto anayeitwa Ifeanyi, alionekana katika video hiyo ambayo ilipostiwa na mwanasheria wa Davido, akicheza muziki wakiwa pamoja na rafiki yake Bobo Ajudua.


Kulingana na ushahidi huo, yaonekana licha ya kuenea na maneno hayo, wawili hao bado wako imara na wanaendelea na maisha yao kama kawaida.

## Funke ukisikia ubinadamu ndo huo

MSANII anayefanya vizuri kwenye filamu za Nollywood, Funke Akindele, amewashangaza mashabiki wake baada ya kumsaidia nyumba mwigizaji mkongwe Kayode Olasehinde maarufu kama 'Pa James'.

Finke alimzawadia nyumba mpya msanii huyo wa zamani baada ya ile ya awali kuzolewa na mafuriko ya maji.

Kutokana na hatua hiyo, watu wengi walijitokeza mitandaoni wakimpongeza mwigizaji huyo wakisema ameonyesha roho ya huruma kwa watu wanaomhitaji.



MAKALA

## MASAHIBU YA MTOTO AYOUB

# Mwenye ualbino aliyefiwa na baba, mama, dada walishatoweka kitambo

- Mwangalizi bibi wa miaka 90, haoni
- Anayempigania binamu asiyejiweza
- Shule alianza miaka 12, aipenda balaa

**Na Mwandishi Wetu,** IRAMBA

AYOUB Ramadhani (16) ni mwenye ualbino anayesoma darasa la tano katika Shule ya Msingi Kizega, (mchanganyiko), iliyopo New Kiomboi, Halmashauri ya Manipsaa Iramba, mkoa Singida.

Ni shule yenye wanafunzi 50 wa mahitaji maalumu kama ualbino, uono hafifu na ulemavu viungo, akiwamo Ayoub kutoka kijijini Kitumbili, kitongoji cha Nkumbo, Manispaa Mkalama, umbali wa kilomita 80.

Ayoub anaishi na bibi wa miaka 90 na kuna binamu, anayemfadhili na kumfuatilia kimaisha, ikiwamo masomo.

**HALI SHULENI**

Siku tatu tangu kufunguliwa shule kutoka likizo oa corona, Nipashe ilipata faragha na Mwalimu Mkuu, Adrea Muna, anayekubali mahudhurio ya wanafunzi ni wastani, isipokuwa wenye mahitaji maalumu wengi hawakuwapo.

Anaeleza wanafunzi 27 sawa na asilimia 40, hawakuhudhuria na anatoa sababu, baadhi wanatoka mbali, akitaja baadhi ya vitongoji kama Iguguna, Kinadili na Mkalama, ambako wazazi na walezi wanahitaji kuwakimu watoto nauli na mahitaji, akitia shaka hawakuwa nayo.

Muna anasema katika likizo ya ugonjwa corona, uchumi wa wakazi wengi wakiwa wakulima zilisimama, kama kipindi masika ambacho wazazi hulalamikia nauli.

Pia, anaieleza shule ya Kizega ni ya serikali na inafadhiliwa na wadau kuwezesha mazingira mazuri kama uzio, umeme, maji, mabweni, magodoro, vitanda na vifaa vya kufundisha, pia mahitaji kwa wenye shida ya uono.

"Ugonjwa wa huu (ualbino) umeleta changamoto kwa wanafunzi hawa. Wengi wakiwa hapa ndio sehemu nzuri na salama kwao kujisomea na kuishi," anasema na kutaja shida kuu ya wanafunzi ni pesa za kurejea shule, akiongeza wanafunzi wanapokuwa shuleni, inakuwa rahisi hata kuwatibu.

**MLEZI WATOTO**

Mlezi (Matroni), Grace Samson (67), anasema wanafunzi wamechelewa kutokana na uchumi duni nyumbani, pia janga la corona limewayumbisha.

Grace anaeleza uhalisia wazazi wengi hawaweki mkazo katika elimu ya watoto, hata kuwachelewesha kurudi kwa wakati baada ya likizo.

Anasema, watoto wanakabiliwa na upungufu wa mahitaji kama sabuni, jambo linalomfanya aiombe serikali ibuni utaratibu wa kuwafuata baada ya likizo, hali itakayowasaidia wazazi masikini wamudu kuwafikisha shule kwa wakati.



Mtoto Ayoub Ramadhani, akiwa katika picha ya pamoja na bibi yake, Amina Mwekwa, kijijini Kitumbili, Manispaa Mkalama, mkoani Singida. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

**MAGUMU YA AYOUB**

Ramadhani Hamisi (32), binamu na mlezi wa Ayoub, alipotakiwa kueleza sababu ya kumchelewesha mwanafunzi huyo masomoni kwa muda, anakiri alikosa nauli, sare na begi mpya zilizohitajika.

Ofisa Elimu Msingi wa Manispaa ya Iramba, Chacha Kehogo, anasema anafahamu matatizo ya wanafunzi wa mahitaji maalumu wanaohitajiwa kurejea shuleni, baada ya likizo, akimtaja pia Ayoub.

Hamisi anaeleza historia ya binamu yake, kwamba alizaliwa akiwa na dada watatu na mdogo wa kiume. Alimpoteza baba tangu alipokuwa na miaka minne.

Anasimulia mama wa mtoto huyo aliishi muda mfupi na kisha aliolewa katika kitongoji kingine, akiwaacha wanawe na bibi yao. Watoto wa kile nao walitawanyika baadaye.

Ramadhani anasema, dada za Ayoub hawajulikani waliko, akibakiwa na tetesi ya kuwapo jijini Dar es Salaam na Arusha. Pia, ni muda mrefu hawajui mama yake aliko.

**KUCHELEWA MASOMO**

Anasema Ayoub alianza masomo ya msingi akiwa na miaka 12, kutokana na hali yake na uhalisia wa uchumi wa familia anayoegemea.

Ramadhani anasema, Ayoub kusajiliwa shule kulitokana na shinikizo la serikali za mitaa, ngazi kitongoji kuwaamuru kumpeleka shule na wakaelekeza shule maalumu anakosoma sasa.

"Amechelewa kurejea shuleni likizo hii, kutokana na uwezo wangu na bibi ni mdogo. Sikuweza kufanya shughuli yoyote wakati wa kipindi cha ugonjwa wa corona, kwani kulikuwa hakuna magulio na wala minada" anasema.

Hamisi, anasema ana familia ya watoto watatu inayohitaji huduma zake na mdogo wa Ayoub, tegemeo lake kiuchumi ni kazi ya udalali wa mbuzi na kuku kwenye minada na magulio ya wilaya hiyo,

Anasema, ili amudu kumrejesha Ayoub shule, alihitaji wastani wa Sh.30, 000 za sare na mahitaji ya Ayoub, kwani hatozwi nauli kwenye magari .

Hamisi anasema corona ilipokuja, shughuli za kiuchumi kama kwenda magulioni na minadani zilisimama na ikamwamisha kipato, hata akashindwa kukamilisha mahitaji ya Ayoub, kurudi masomoni.

Kuhusu usalama wake Ayoub, anasema kutokana na hali yake huwa anamsisitiza asicheze mbali na nyumbani, kwani kijiji chao kimezungukwa na msitu na mapori, hali inayondoa mazingira salama kwake.

"Ayoub hajawahi kupata tatizo lolote kama la kushambuliwa kutokana na hali yake. Mara zote tunamsihi akae karibu na nyumbani na bibi yake.

"Hatumpi kazi za kwenda kuchunga peke yake, kwani sio salama kwakwe. Anapenda muda wote awepo shuleni huko ndio salama kwake," anasema

**BIBI AYOUB**

Amina Mwekwa (90), ni Bibi wa Ayoub aliyeanza kumlea mtoto huyo tangu alipompoteza baba yake, akiwa na ndugu zake wengine kwa kushirikiana na mama yao.

Bibi huyo anasema mama wa mtoto alitoweka kusikojulikana, hali inayomuacha katika jukumu la ulezi peke akiwa na umri wa uzee.

Hata hivyo, Bibi Amina amepoteza uwezo wa kuona, hivyo anaishi kwa msaada wa wajukuu zake, akiwemo Hamisi. Kabla alikuwa mkulima.

Anamtetea mjukuu wake kwamba, anapenda sana kusoma na amekuwa akilalamika kila wakati anahitaji kurudi shuleni, ila shida inayomkabili ni nauli usafiri na sare, kwani kipato cha mjukuuu wake Hamisi hakitoshelezi kuendesha maisha ya familia yote.

**HAIBA YAKE**

Mtoto Ayoub ni mwenye aibu sana na muda wote katika mazungumzo na Nipashe, alikuwa anainamisha uso wake chini, ana alipoulizwa alivyoathiriwa nalikizo ya corona, anasema imemuumiza sana.

Asema kuwa ameumia sana na bado alikuwa anaendelea kuumia, kwani hapendi kukaa nyumbani, ila changamoto yake ya nauli na sare za shule hazijapata ufumbuzi.

Mtoto huyo anaeleza ridhaa yake, hapendi shule iwe inafungwa, kwani awapo shuleni huwa anapata faraja anapokuwa na watoto wenye hali kama yake na salama kwa kupata lishe na kulala sehemu nzuri kimazingira.

"Shuleni kwetu ni pazuri. Kuna umeme, maji na chakula cha uhakika kuliko nyumbani hapa. Napata muda wa kujisomea na nakula vizuri niwapo shuleni, natamani shule isiwe inafungwa milele. Napenda niishi shule tu," anasema Ayoub.

Kuhusu masomo ayapendayo, anataja masomo ya Sayansi, Hisabati na Kiswahili na ndoto yake kuwa mwalimu baadae.

"Najisikia vibaya sana kukosa shule. Likizo ya corona imenifanya niwe mnyonge nyumbani. Naumia sana, nawasumbua nyumbani kila siku wanipeleke shuleni, ila walikuwa wanasema wanatafuta hela kwanza ndio nirudi shuleni," anasema.

Kilio cha Ayoub, kilihitimishwa na ziara ya mwanahabari, aliyeamua kukamilisha mahitaji yote na alirejea masomoni, Jumatano iliyopita



Nyumba anayoishi Ayoub Ramadhani na bibi yake, Amina Mwekwa.

MAKALA

# Mawakili wapya na fursa ya kusaka ajira vijijini

Na Moshi Lusonzo

MAWAKILI 601 jana wameapishwa na kuthibitishwa na Jaji Mkuu, Profesa Ibrahim Juma, hivyo hatua hiyo inawapa nafasi ya kuanza hatua nyingine muhimu ya kusaka ajira.

Katika hafla hiyo iliyofanyika kwa njia ya mtandao, Jaji Ibrahim Juma, amewakumbusha mawakili hao kwenda kufanya kazi zao kwa kuzingatia kanuni, maadili na mabadiliko ya teknolojia katika utendaji wao wa kazi.

Hata hivyo, amewataka wanasheria kukubali kubadilika kwa kuendana na kasi ya mabadiliko ya kiuchumi, na kuachana na dhana za kizamani kwamba kada hiyo ni ya watu maalum.

Profesa Juma, anasema kutokana na wingi wa wanasheria nchini na mabadiliko ya kasi ya kiuchumi, ni muhimu kwa mawakili hao kuanza kutafuta fursa vijijini badala ya kung'ang'ania mijini ambako kwa sasa hakuna nafasi za ajira.

"Jitayarisheni kufanya kazi katika karne yenye ushindani mkubwa, wakati wa uhuru kulikuwa na ajira nyingi, lakini kwa sasa kuna changamoto ya kupata kazi. Badilikeni kwa kutafuta fursa nje ya miji ambako kuna mahitaji mengi ya kisheria," anasema Jaji Mkuu.

Anasema wakati wa wanasheria hao kufikiria kufungua kampuni kwa lengo la kupata wateja katika migodi na serikalini, imefika mwisho kwani sasa hakuna njia ya mkato.

"Zamani mawakili wanapomaliza masomo waliunda kampuni zao kwa ajili ya kufanya kazi na benki kuu au migodi ya madini, lakini sasa hali hiyo haipo ni lazima kubadilika ili kutafuta njia nyingine inayofaa," anasisitiza.

Kauli hiyo ya kiongozi mkuu wa Mahakama, inaungwa mkono na wakili mpya kijana, Rehema Mmanga, ambaye anasema wito huo umemfanya kutafakari na kujipanga upya katika kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira.

Anasema, ni ukweli kwamba maeneo ya vijijini kuna fursa nyingi ya kupata kazi, kutokana na kuwa na watu wengi wanaohitaji huduma ya kisheria, lakini wanaikosa baada ya mawakili kubaki mijini.

Rehema, anaeleza kwamba anafikiria kutekeleza wazo hilo kikamilifu kwa kwenda kuwatumikia jamii ambazo ziliachwa nyuma kutokana na sababu mbalimbali.

"Mimi kama wakili mpya, namshukuru Jaji Mkuu kwa kunifungua macho baada ya kunionyesha fursa kubwa ambazo tulikuwa hatuioni, naamini vijijini kuna watu wanaohitaji huduma za kisheria lakini kutokana na umbali wa kwenda kuwapata au kutokuwa na ufahamu wameikosa," anasema Rehema.

Anaeleza ni lazima wao kama wanasheria vijana kuonyesha wanakwenda sambamba na teknolojia ya hali ya juu ambayo inafanya dunia kuwa moja pamoja na kurahisisha utendaji wa kazi.

"Sisi mawakili vijana tunalazimika kutofautiana na wale wa zamani, ni lazima tukimbie haraka kufuatana na teknolojia inavyotaka, tunaweza kufanya kazi sehemu yoyote au kujiingiza katika ujasiliamali bila kuathiri taaluma yetu," anaongeza kusema.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Profesa Juma, tatizo la mawakilli kukosa kazi linaikabili nchi nyingi zikiwemo zile zenye uchumi wa juu, kutokana na kuwepo na idadi kubwa ya wanasheria kuliko mahitaji ya soko.

Kwa upande wa wakili Idd Rashid, ameseka hakuna waanasheria wanaokataa kwenda kufanya kazi vijijini, ila wanashindwa kufanya hivyo kutokana na changamoto za kimazingira.

Anazitaja changamoto hizo kuwa ni uhaba wa soko, umbali wa mahakama na uelewa hafifu wa wananchi katika sheria.

Rashid anasema mawakili wengi wamejazana maeneo ya mijini kutokana na kuwa na soko kubwa na miundo mbinu ya kimahakama kuwa rafiki.

"Unapofanya kazi mjini unakutana na watu wenye uelewa mpana wa kisheria na miundombinu ya kufikia vyombo vya sheria kuwa karibu, hii inawapa nguvu mawakili kuamua kufanya kazi mjini kuliko vijijini," anasema Rashid.

**ONYO KWA MAWAKILI**

Pamoja na ushauri huo, Jaji Mkuu hakusita kuwaonya mawakili hao wapya kuwatumikia wananchi bila kutafuta maslahi binafsi, badala yake wazingatie kutoa haki kwa wateja wao.

Prof. Juma, anasema ifikie wakati wasomi hao wa sheria wasisubiri haki ipatikane mbele ya mahakama, badala yake wanaweza kutumia ushawishi wao wa kielimu kutatua matatizo ya wananchi kabla ya kufika katika chombo hicho.

Anasema kazi ya uwakili ni ngumu na inayobeba dhima ya uaminifu, kutokana na wananchi kuiamini na kuwapa taarifa zao za siri ambazo hazipaswi kutoka nje.


"Kazi ya uwakili ni kazi ya kuaminiwa na yenye uaminifu wa hali ya juu, mwananchi anakuamini na kukupa taarifa ambazo ni za siri, lazima kuzihifadhi na kutoa haki. Lazima kueshimu maadili, katiba na sheria, kwani mmepewa nafasi na utashi ambao unaweza kutumia vizuri au vibaya," anazidi kueleza.

Prof. Juma anakemea vitendo vya baadhi ya mawakili kupokea rushwa ili kumnyima haki mwananchi, kwa sababu kufanya hivyo atakua umekiuka maadili na sheria za nchi.



Mmoja wa mawakili wapya kijana, Rehema Mmanga

**"Mimi kama wakili mpya, namshukuru Jaji Mkuu kwa kunifungua macho baada ya kunionyesha fursa kubwa ambazo tulikuwa hatuioni, naamini vijijini kuna watu wanaohitaji huduma za kisheria lakini kutokana na umbali wa kwenda kuwapata au kutokuwa na ufahamu wameikosa," anasema Rehema.**



Jaji Mkuu wa Tanzania, Ibrahim Juma




Mamia ya wahamiaji kutoka Syria wamekimbilia Iraq kutokana na machafuko nchini humo. **PICHA: MTANDAO**

# WHO kuchunguza chanzo virusi vya corona Beijing

**BEIJING, China**

WATAALAMU wawili wa Shirika la Afya Duniani (WHO), wamekwenda Beijing nchini China kuchunguza chanzo cha virusi vya Corona.

Wataalamu hao, akiwamo wa afya ya wanyama na daktari wa kuchunguza kiini cha magonjwa watakutana na wenzao kutoka China ili kuchunguza namna virusi hivyo vilivyotoka kwa wanyama na kuingia kwa binadamu.

Wanasayansi wanaamini kuwa asili ya virusi vya Corona ni wanyama aina ya popo na baadaye virusi hivyo viliambukizwa kwa wanyama wengine na kuwafikia binadamu.

Mji wa Wuhan ndiyo ulikuwa kiini cha virusi hivyo mwaka jana, lakini uchunguzi wa hivi karibuni umeonyesha kuwa huenda mlipuko huo ulianzia sehemu nyingine.

China imepiga marufuku biashara ya wanyama pori na kufunga baadhi ya masoko nchini humo ili kuzuia kusambaa kwa virusi hivyo.

**DW**

# EU yaipinga Marekani adhabu ya kifo

**BRUSSELS, Ubelgiji**

UMOJA wa Ulaya (EU) unapinga vikali uamuzi wa Marekani wa kuanza tena kutekeleza adhabu ya kifo baada ya kusitishwa kwa miaka 17.

Serikali ya Marekani iliamua karibu mwaka mmoja uliyopita kurejesha adhabu ya kifo ambayo ilitekelezwa mara ya mwisho mwaka 2003.

Msemaji Mkuu wa EU, Josep Borrell, ameitaka Marekani kufikiria upya kuhusu uamuzi huo na kutoendelea na mipango ya mauaji iliyopangwa kufanyika kesho kutwa.

Mwezi Juni, Mahakama za Marekani ziliidhimisha matumizi ya sindano zenye sumu dhidi ya wahalifu sugu na tayari maofisa wamepanga kutumia njia hiyo mwezi Julai na Agosti.

Kesi nyingi za uhalifu nchini Marekani husikilizwa na mahakama za majimbo lakini baadhi kwa ngazi ya kitaifa kama vile uhalifu wa kueneza chuki ama kesi zinazofanyika ndani ya jeshi.

**DW**

# Mawaziri sita wajiuzulu Sudan

**KHARTOUM, Sudan**

WAZIRI Mkuu wa Sudan, Abdullah Hamduk, amefanya mabadiliko katika baraza la mawaziri baada ya kuwapo kwa shinikizo la kutaka mageuzi ya kisiasa.

Kwa mujibu wa taarifa ya serikali, Waziri Mkuu huyo amekubali kujiuzulu kwa mawaziri sita wakiwamo waziri wa mambo ya nje, fedha, kilimo, nishati na uchukuzi.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa, baada ya kujiuzulu kwa mawaziri hao, wizara hizo sasa zitasimamiwa na manaibu wake hadi uteuzi mpya utakapofanyika.

Mabadiliko hayo yanafanyika baada ya mwishoni mwa mwezi Juni, maelfu ya waandamanaji kushinikiza kufanyika mageuzi ya haraka ya kisiasa ikiwamo kubuniwa kwa Bunge, vikosi vya usalama na uwapo wa idara huru ya mahakama.

Nchi hiyo imeshuhudiwa wimbi kubwa la mabadiliko ya kisiasa baada ya mwezi Aprili mwaka jana, kung'olewa madarakani kwa Rais Omar al- Bashir.

**DW**

# Mbwa 'wafukua makaburi ya watoto' Msumbiji

**MAPUTO, Msumbiji**

MBWA wanaozurura mtaani nchini Msumbiji wamekuwa wakifukua makaburi ya watoto katika mji wa Chimoio, kituo cha runinga cha Miramar kimeelezwa.

Mama mmoja alisema siku chache zilizopita baada ya kumzika mtoto wake alikwenda makaburini kufanya usafi na alipofika alikuta mbwa wakiwa wamefukua kaburi na kula maiti yake.

Ripoti za vyombo vya habari nchi humo zinaonyesha vipande vya nguo, mifupa na nyama ya binadamu iliyotapakaa katika eneo la makaburi ya umma.

Mwandishi wa kituo cha Miramar ameiambia BBC kwamba, katika kipindi cha wiki tatu makaburi 343 ya watoto yalifukuliwa na mbwa. Wakazi walisema mbwa hao wamekuwa tatizo la kila siku na kwamba hali hiyo imekuwa mbaya zaidi katika miezi ya hivi karibuni kwa sababu ni watu wachache wanaoruhusiwa kufika katika maziko hayo kutokana na mlipuko wa virusi vya corona

Janga la virusi vya corona pia limewafanya watu kupoteza kazi na huenda hawana uwezo wa kukimu familia zao wala kuwalisha wanyama wao.

Wenyeji wa eneo hilo walisema, hatua ya makaburi ya umma kutozungushiwa huenda imechangia tatizo hilo.

Mamlaka ya mji wa Chimoio, ambao ni makao makuu ya mkoa wa Manica karibu na mpaka wa Zimbabwe, haikuwapo kutoa tamko kuhusiana na tatizo hilo.

**BBC**

# HADITHI

# Mauaji Harusini-20

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awe navyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele.

Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.

Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

**Na Adam Fungamwango, (0716 350534)**

"Ila kwa upande wangu wewe ndiyo sababu. Mimi muda wote nawaza kutaka kuongea na wewe. Huwa nafurahi sana nikikuta meseji yangu, hasa pale siku za mwanzo ulipotoka huku, lakini baadaye nikaona umenisahau."

Eddy alicheka kidogo na kuongea. "Wewe hunishindi mimi kukuwaza."

"We mimi nakushinda, siku hizi hunitumii meseji, sijui unasema una kibarua kimekuweka bize, siku ile ulipotoka kwangu, ilikuwa kila siku asubuhi unanitumia meseji, basi nilikuwa nafurahi sana, siku nisipoona nawaza kuna nini? Lakini siku hizi..."

Hapo Eddy alijua kuwa yalikuwa ni malalamiko. Malalamiko yaliyotokana na mazoea. Anakumbuka siku ile alipoalikwa na Shani, ilikuwa asubuhi ni lazima amtumie meseji ya kumsalimia na kumtania kama kawaida yake, kabla ya kufanya chochote.

Tayari alijua ana kazi ya kufanya.

"Kwa nini ukiona meseji yangu unafurahi sana?" Lilikuwa ni swali ya uchokonozi kutoka kwa Eddy.

"Mimi nahisi upendo, wewe unahisi nini?" Lilikuwa ni jibu lililochanganyikana na swali. Tena la mtego.

"Upendo si ndiyo mapenzi? Au mimi nachanganya madawa?" Hilo lilikuwa ni swali jibu, halafu lililotengenezwa kiufundi kabisa na Eddy.

"Mmmh, hapo mimi sasa sielewi, ndiyo maana nimekuuliza wewe." Shani alikwepa swali la kiufundi.

Eddy alijua hilo, akaangua kicheko na na kusema.

"Hahahaha, upendo ndiyo hayo hayo mapenzi, ila mimi naona upendo umezidi kwako. Yaani nakupenda sana."

Kulitokea ukimya wa ghafla baada ya maneno hayo kwa wote wawili. Baada ya nusu dakika Shani aliuvunja na kuguna

"Duh."

"Mbona umeshtuka?" Eddy aliuliza.

"Hapana. Nimefurahi tu." Shani alijibu.

"Unanicheka eee, poa tu Mungu yupo."

"Sijakucheka bwana. Nimefurahi tu, kwa sababu hata mimi najisikia kama wewe." Shani alijibu na kushusha pumzi ambayo hata Eddy aliisikia kwenye simu yake.

"Pole sana." Eddy aliongeza.

"Kwa nini sasa hukuniambia sasa tokea mwanzo ulivyoanza kujihisi hivi kwangu mimi?" Shani alionekana bado kutaka kujua kitu.

"Shani, kila kitu kina muda wake, ilibidi kwanza nijidhihirishe kama nakupenda au nakutamani tu. Ila sasa nimeamini kuwa nakupenda kutoka rohoni."

"Okay, nimekuelewa Eddy."

"Poa, basi nikutakie mchana mwema."

"Okay kazi njema Eddy."

"Na kwako pia."

"Nakupenda." Kwa mara ya kwanza Shani alitamka neno hilo kwa Eddy.

Kwa upande wake Eddy alitabasamu na kuona sasa kazi ya kumtia mkononi mrembo Shani ilikuwa imekamilika. Kwa muda mfupi tu walipoonana, aliondokea kumhusudu sana.

"Nami pia nakupenda sana." Eddy alijibu.

"Nakuomba Jumamosi uje kwenye hoteli ya ABC Club Mbezi Beach ili tufurahi kwa pamoja, tujipongeze."

"Omba kingine mpenzi, hilo limepita bila kupingwa." Eddy alijibu, maongezi yakaisha na kukata simu zao.



*******************************************

Ilikuwa ni moja kati ya hoteli za kisasa zilizojengwa maeneo ya Mbezi Beach. ABC Club ilikuwa ni moja kati ya hoteli zilizopendwa mno na watu wa maeneo hayo na sehemu zingine jijini Dar es Salaam.

Ni nyumba ya hoteli ghorofa mbili. Pamoja na kuwa na vyumba vingi vya hoteli, lakini mbele ya jengo hilo kuna baa ya kisasa, pamoja na mgahawa mkubwa wenye vyakula vitamu, hususan samaki, chakula ambacho ndicho hupendwa sana na wateja wengi.

Kama kawaida hoteli hiyo siku hiyo ilipokea wateja wengi, ambao ni wale wale wa siku zote, lakini baadhi yao ni wapya.

Mmoja wa wateja wapya, alikuwa amekaa pembeni upande wa Kaskazini Magharibi. Alikaa kwenye kiti ambacho kilikuwa kinatazama mlango mkuu upande wa Kusini Mashariki.

Aliishi kwa kanuni zile zile za kipelelezi. Zile zile za kikachero. Ndiyo maana hakukaa sehemu hiyo kwa bahati mbaya. Au kwa sababu tu amekikuta kiti kiko wazi.

Mara nyingi sehemu kama baa, hoteli, au sehemu yenye mikusanyiko ya watu na hasa kwenye kumbi, watu wengi ambao wamepitia mafunzo ya upelelezi, au yanayofanana na hayo, hawakai hovyo tu.

Hukaa maeneo ya pembeni ambayo huangalia geti au mlango mkuu. Lengo ni kujua, au kuhisi mtu yoyote mbaya anayeingia ili kujiokoa yeye mwenyewe au kuokoa watu wengine kabla adui hajafanya kitu chochote kibaya.

Mara nyingi watu wa intelejensia wana uwezo mkubwa wa kunusa au kuhisi hatari, lakini pia kumhisi mtu ambaye si wa kawaida mara tu wanapomuoa. Na hii huwezi kufanya kama utakuwa umekaa umelipa geti au mlango mgongo.

Yupo mtu wa kawaida tu, aliwahi kujiokoa kwa kukaa macho yake yakiangalia mlango mkuu na wakaingia watu wawili kwenye baa aliyokuwa anakunywa. Lakini jinsi walivyoingia tu, alihisi hawakuwa watu wazuri kwa sababu walikuwa wamevaa makoti marefu na mawani mweusi, tena ikiwa usiku. Jamaa aliihisi hatari akainua na kuondoka papo hapo. Kesho yake akaambiwa kuwa dakika 10 tu baada ya kuondoka, walivamiwa na majambazi na waliwapora wateja, pamoja na kuchukua pesa za mauzo.

Huyo ni mtu wa kawaida tu. Watu wa intelejensia wao wanaenda mbali zaidi na kuweza kumtambua adui ambaye hata kwa macho ya kawaida tu hayaonyeshi kuwa ni mtu mbaya.

Eddy Kamal, pamoja na kwamba alikuwa kwenye ahadi ya kimapenzi, lakini akili yake bado iliendelea kuwa ni ya kipelelezi na kiintelejensia zaidi. Kwa sababu tayari ameshazoea maisha hayo na kuna wakati mpaka mwenyewe anajiashangaa na kujicheka kwa sababu hata anakuwa kwenye hali hiyo hata kwenye maeneo ambayo hayahitajiki.

Hata hivyo, huwa anakumbuka ile kanuni ya 'Usimuamini mtu yoyote, au kitu chochote hata kama ikiwa maiti.'

Alifika hapo majira ya saa sita kasoro dakika kumi hivi. Lango awe hapo tangu saa sita kamili, huku wakiwa wamehidiana na Shani wawe hapo saa saba mchana kwa ajili ya kupata chakula cha mchana, na kufurahia kukubaliana kuwa wapenzi.

Simu ya mwisho aliyowasialiana na Shani, alikuwa nyumbani kwake Kijitonyama na kumwambia kuwa ameanza kujiandaa kuoga, ili aweze kufika huko. Wakati huo yeye alikuwa anafungua mlango wa gari ili kuwahi ahadi.

Kila mtu aliendelea na shughuli zake kama kawaida. Kuna waliokuwa wakinywa vinywaji vikali kama vile bia, na pombe kali. Wapo waliokuwa wakinywa vinywaji baridi kama soda na maji.

Wengine walikuwa hapo kwa ajili ya chakula cha mchana. Wengine wakinywa supu ya nyama za wanyama mbalimbali, wengine supu ya samaki.

Cha zaidi ni kwamba asilimia 90 ya waliokuwa humo ndani, walikaa wawili wawili, mwanaume na mwanamke. Wengi kila mtu alikuwa na mpenzi wake. Eddy ni mmoja wa wateja ambao alikuwa peke yake.

Tena mwanaume alikuwa peke yake, waliobaki walikuwa ni wanawake watatu waliokuwa wamekaa peke yao kila mmoja.

Sijui nao walikuwa wanawasubiri wapenzi wao kama Eddy au vipi? Dada mmoja nadhifu aliyevaa sare alifika kwenye meza yake na kumuuliza angekunywa kinywaji gani.

"Bado namsubiri mgeni wangu, lakini hebu niletee maji ya Kilimanjaro chupa kubwa." Aliagiza.

Kinywaji kilipofika alianza kunywa taratibu, akivuta muda wa kumpokea mgeni wake, ambaye hapo yeye alikuwa ni mwenyeji kuliko anayemsubiria.

Muziki mororo ulitumbuiza kutoka kwenye spika zilizokuwa pembeni. Macho yake yalikuwa yakiangalia kila kitu kilichokuwa humo, mpaka alipojidhihirisha kuwa ni salama kama kawaida yake.

Kulia kwake kulikuwa na meza ya baba mmoja kibonge mtu mzima, aliyekuwa amekaa na mpenzi wake, mithili ya baba na binti yake wa tatu au wa nne.

Kilichomvutia Eddy ni maneno ya mzee huyo aliyokuwa akiyaongea kwenye simu iliyoonekana anaongea na mkewe.

"Nimepata safari ya ghafla mke wangu ya kikazi kwenda Morogoro, yaani leo sitorudi hadi kesho jioni."

Na baada ya kumaliza kuongea, akamgeukia mpenzi wake.

"Kwisha kazi mke keshaingia kingi, yaani leo ni kula bata tu hadi kuku waone wivu. Leo tutalala hapa hapa hotelini hadi kesho jioni."

Eddy alimtupia jicho la wizi, akatabasamu. Wakati huo mhudumu mmoja wa kiume alifika na kuwaongezea vinywaji wapenzi hao.

Wakati akiwa wamevuta hatua tano tu, ghafla kuna kitu kilianguka kutoka kwenye mfuko wake kwa bahati mbaya.

Ni Eddy tu ndiye aliyekiona. "Ni leso, au pesa?" Alijiuliza. Haraka akili ikamtuma ajidhihirishe kwanza kabla ya kumwita aje kuchukua kitu alichoangusha.

Aliinua kama vile anayetaka kwenda msalani, akavuta hatua chache tu, haraka akainama na kuokota kitu kile kabla yoyote yule hajaona.

Akakaa kwenye kiti. Ilikuwa ni kifuko kidogo cha nailoni kilichofunguliwa. Kilikuwa na unga wenye rangi ya kahawia ambao tayari ulikuwa nusu. Akahisi hatari. Akatoa leso mfukoni na kukiweka kifuko kile katikati ya leso yake ili kuzuia unga usitoke na kugusa mikono yake. Akasoma maandishi yaliyo kwenye kifuko hicho.

Akatabasamu. Halikuwa tabasamu halisi. " Hii ni sumu" Alijisemea moyoni.

***Itaendelea Jumamosi***

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA/MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA,** Nyumba inauzwa ina ghorofa moja, ina godown ina fremu 10 na ina eneo kubwa wazi, ipo Dar es Salaam. Mawasiliano 0757 079057

## *NIPASHE NI JIBU LAKO*

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2 Katika mahakama ya mwanzo**

**MJINI-MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No;179/2020**

Ombi la OSCAR EDWARD MTEY NA MAGRETH KENEDY.Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ALFRED EDWARD MTEY Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 15/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 10/07/2020.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No;178/2020**

Ombi la MWASITI JUMA MISOTI,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MKOLA ALLY KAMBANGA Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 13/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 09/07/2020.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

---

**KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI**

**CYPRIAN PIUS LYANGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji aina ya TVS KING yenye namba za usajili MC.325 BGS.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.
Taarifa ya polisi **MBE/MBE/R-B/519520/2020.**

---

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

---

***Kwa Habari Motomoto***

***usikose Gazeti lako la***

***Nipashe kila siku***

***Tupigie***

***0782253676***

---

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# SOLSKJAER

## AWAPA NENO WACHEZAJI MAN UNITED

**MANCHESTER, England**

OLE Gunnar Solskjaer amewashauri wachezaji wa Manchester United kutumia maneno ya Paul Pogba kama hamasa ya kuwasukuma kwenye kuwania taji la Ligi Kuu England.

United waliendelea kutopoteza mchezo na kufikisha mechi 17 wakati wakipata ushindi wa 3-0 dhidi ya Aston Villa Alhamisi.

Pogba alisema "ubora" kwa United ndio unaoweza kuwafanya washinde taji la Ligi Kuu ambalo kwa mara ya mwisho walilitwaa msimu wa 2012-13.

Kocha huyo wa United, Solskjaer anajiamini kwamba klabu inaweza kurudi juu, na ni suala la mchezaji mmoja mmoja kujituma kwa bidii.

"Nina uhakika United watatoa changamoto na kurudi tena kwenye ubora wao wa kushinda ligi," alisema.

"Wakati kitu kitakwenda kutokea kila mmoja wetu anatakiwa kujituma katika kila mchezo na kuhakikisha tunafanya vizuri kwa siku za usoni na hilo ndio pekee litakalotuwezesha kufika mbele."

United ambayo Jumatatu itacheza na Southampton wamepitwa pointi moja na Leicester City iliyopo nafasi ya nne.



## CONTE AKATAA KUWALAUMU NYOTA WAKE

**MILAN, Italia**

KOCHA wa Inter Milan, Antonio Conte, amekataa kuwalaumu wachezaji wake baada ya kuongoza mechi na mwisho wa mchezo wakalazimishwa sare ya 2-2 dhidi ya Hellas Verona, Alhamisi.

Nerazzurri walikuwa wanaongoza hadi zikiwa zimesalia dakika tano mpira kumalizika pale kwenye dimba la Marcantonio Bentegodi, lakini Miguel Veloso alionesha maajabu kwa kusawazisha na kuwapa wenyeji pointi moja.

Inter ilianza kwa uongozi wa mapema kipindi cha pili shukrani kwa bao la Antonio Candreva na lile la kujifunga la Federico Dimarco kabla ya Darko Lazovic kuipa bao moja Verona.

Ni mara ya pili ndani ya siku tano baada ya Inter kufungwa mabao 2-1 na Bologna Jumapili, lakini Conte hakutaka kuwalaumu wachezaji wake.

"Kwa suala la kujituma, njaa ya mafanikio na kujitoa, siwezi kuwalaumu wachezaji," alisema akinukuliwa na Sky Sport Italia.

"Tusisahau, tulicheza dhidi ya Verona kikosi kile kilikuwa kwenye presha kubwa na walitupa wakati mgumu. Nafikiri Inter tulibanwa."

## PSG KUANZA KUTETEA TAJI KWA METZ

**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Paris Saint-Germain itaanza kampeni ya kutetea taji la Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, nyumbani dhidi ya Metz baada ya ratiba ya ligi hiyo kwa msimu ujao wa 2020-21 kutangazwa .

Raundi ya kwanza ya ligi hiyo itaanza wiki ya Agosti 22 hadi 23, na msimu huo utamalizika Mei 23 mwakani.


PSG walipewa taji la Ligi Kuu Ufaransa kwa mara ya saba mfululizo ndani ya misimu nane baada ya msimu wa 2019-20 kuhitimishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Timu za Amiens na Toulouse zimeshushwa daraja, huku Lorient na Lens zikiwa zimepanda kutoka Ligi Daraja la Pili.

Lorient wataanza na Strasbourg kwenye mchezo wake wa kwanza kwenye ligi hiyo, huku Lens watafungua msimu na Nice.



# PELLEGRINI
## APEWA MIKOBA REAL BETIS



**MADRID, Hispania**

MANUEL Pellegrini atachukua mikoba ya kuwa kocha mkuu wa Real Betis kwa msimu ujao, klabu hiyo imethibitisha juzi Alhamisi.

Kocha huyo wa zamani wa Manchester City na Real Madrid, Pellegrini amekubali kusaini mkataba wa miaka mitatu pale kwenye dimba la Benito Villamarin.

Raia huyo wa Chile mwenye umri wa miaka 66 alikuwa hana timu tangu alipofukuzwa West Ham Desemba mwaka jana.

Betis walimfukuza kocha wao Rubi baada ya mechi tatu tangu kuanza upya kwa msimu uliosimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, na sasa wapo nafasi ya 14 kwenye msimamo.

Mkurugenzi wa michezo wa klabu hiyo, Alexis Trujillo amepewa jukumu la kuwa kocha wa muda hadi mwishoni mwa msimu huu na ameshapata ushindi mara mbili katika mechi tano.

Ingawa mafanikio makubwa ya Pellegrini aliyapata kwa kubeba taji la Ligi Kuu England na lile la EFL msimu wa 2013-14 akiwa na City, amekuwa na mafanikio pia kwenye LaLiga kipindi alichokuwa kule.

Aliiongoza Villarreal kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2005-06 na kumaliza nafasi ya pili kwenye LaLiga miaka miwili iliyopita.

Pellegrini hakupata taji lolote msimu wa 2009-10 akiwa na Madrid kabla ya kuchukua mikoba ya kuinoa Malaga.

## POGBA: NITAMSAIDIA GREENWOOD KUFIKA JUU

**MANCHESTER, England**

PAUL Pogba ameahidi kumsaidia Mason Greenwood kufika juu baada ya kinda huyo wa Manchester United kufunga tena dhidi ya Aston Villa.

Greenwood mwenye umri wa miaka 18, alifunga kwa shuti kali la nje ya 18 wakati United wakiibuka na ushindi wa 3-0 pale kwenye dimba la Villa Park na kufikisha mabao manne katika mechi tatu.

Ni mchezaji wa pili kijana wa United kufunga katika mechi tatu mfululizo za Ligi Kuu baada ya Wayne Rooney.

Pogba, ambaye alifunga bao la tatu la United kumaliza ukame wa miezi 15 bila bao la Ligi Kuu, amefurahishwa na kiwango kinachoonyeshwa na Greenwood hadi sasa na mshindi huyo wa Kombe la Dunia anafikiri kuna mengi zaidi yanakuja.

"Ni vizuri sana," alisema Mfaransa huyo akiiambia Sky Sports baada ya kucheza kwa pamoja na Greenwood.

"Napenda kumwona akicheza mbele, nafurahia utoto wake na nitamsukuma kwenda juu.

"Ana vingi vya kufanya tena. Anaweza kufanya zaidi kuliko kile anachokifanya sasa. Ana kipaji cha hali ya juu na anaweza kucheza kwenye timu hii."



## TORRES ATAJWA KUMRITHI SANE

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester City imemfanya nyota wa Valencia, Ferran Torres, kama kipaumbele chao cha usajili, kwa mujibu wa Cadena SER.

Hata hivyo, City inaweza kukabiliwa na upinzani kutoka kwa Chelsea ambao nao wanamtaka.

Torres mwenye umri wa miaka 20, amekuwa akihusishwa na klabu kadhaa za Ulaya baada ya kuonyesha kipaji cha kuvutia pale Valencia, ambako alikulia hapo kutoka timu ya vijana.

City wanataka kumsajili Torres kwa ajili ya kuziba pengo la Leroy Sane, ambaye amejiunga na Bayern Munich.

Torres mkataba wake wa sasa pale Valencia unamalizika mwaka 2021, na pia alikuwa akihusishwa na Liverpool, Manchester United, Juventus na Borussia Dortmund.

Nyota huyo alifunga mabao sita na kutoa pasi za mwisho saba kwenye mechi 41 katika mashindano yote msimu huu.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# IBRAHIMOVIC HAJUI HATIMA YAKE MILAN

●●●Mshambuliaji huyo raia wa Sweden asema anacheza kwa ajili ya kushinda mataji na sio...

**MILAN, Italia**

ZLATAN Ibrahimovic amebainisha kwamba ana shaka kubwa kama ataendelea kubakia katika klabu ya AC Milan kama hali haitabadilika.

Ibrahimovic alirudi Milan, ambako awali alishinda taji la Ligi Kuu Italia, Scudetto mwaka 2011, kama mchezaji huru Januari, mwaka huu baada ya kuondoka kwenye Ligi Kuu Marekani (MLS), katika Klabu ya LA Galax,y lakini kuna mashaka juu ya majaliwa yake baada ya msimu huu wa 2019/20.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 38 amefunga mabao sita tangu arudi Milan, na kuwasaidia Rossoneri hao, walioshinda Ligi ya Mabingwa Ulaya mara saba kuwa na nafasi ya kufuzu Kombe la Europa msimu ujao.

Milan wapo nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu Italia wakipitwa pointi mbili na Roma na mabingwa wa kombe la Italia, Napoli baada ya mechi 31.

Licha ya Milan sasa kuwa kwenye kiwango bora, lakini kocha wake mkuu, Stefano Pioli nafasi yake itachukuliwa na Ralf Rangnick raia wa Ujerumani msimu ujao.

"Ibra anacheza kwa ajili ya kushinda kitu fulani au kubakia nyumbani," alisema Ibrahimovic akiliambia gazeti la La Gazzetta dello.

"Ibra siyo mchezaji wa kucheza Ligi ya Europa na Milan sio klabu ya kucheza kwenye Ligi ya Europa.

"Ibra yupo hapa, Ibra yupo kwa ajili ya kucheza na kushinda mataji na si vinginevyo, hivyo sina uhakika sana kama nitaendelea kubakia hapa kwa msimu ujao.

"Sijajua wapi nitakwenda, lakini uwezekano wa kubakia hapa ni mdogo zaidi kwangu."

## KWA UFUPI

**GUARDIOLA AMTAKA ALABA**
KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, anajiandaa kumsajili beki wa kushoto wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Austria, David Alaba, ambaye ana umri wa miaka 28, katika majira ya joto. ***(Mirror)***

**BRUYNE NJIA PANDA**
WAKALA wa Kevin de Bruyne amesema kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji ambaye ana umri wa miaka 29, hataondoka Manchester City katika majira ya joto mwaka huu, kama adhabu yao ya kushiriki mashindano ya Ulaya itaondolewa. ***(Sporza - in Dutch)***

**DIER AITEGA SPURS**
BEKI wa Tottenham, Eric Dier (26), anataka kulipwa zaidi ya mara mbili ya mshahara wake wa sasa wa pauni 60,000 kwa wiki ili asaini mkataba mpya na klabu hiyo. Mkataba wa sasa wa nyota huyo wa Timu ya Taifa ya England umebakiwa na chini ya miezi 12. ***(Mail)***

**STONES AIPENDA CITY**
BEKI wa Timu ya Taifa ya England, John Stones (26), hafikirii kuondoka Manchester City, licha ya hatima yake ndani ya klabu hiyo kutofahamika. ***(Mail)***

**BARCA YAMWINDA GARCIA**
KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema anaamini beki Mhispania, Eric Garcia (19), atakataa 'kishika uchumba' kutoka Barcelona na kusaini mkataba mpya na klabu hiyo ya England. ***(Times - subscription required)***

**MAGALHAES AGOMBEWA**
EVERTON inatarajia kukutana na ushindani katika kuwania saini ya beki wa Lille, Gabriel Magalhaes (22), baada ya klabu nyingine inayoshiriki Ligi Kuu England kuwasilisha ofa ya kumwania Mbrazili huyo katika dakika za lala salama. ***(Sky Sports)***

**MARTINEZ KUBAKI ARSENAL**
ARSENAL imesema inataka kuhakikisha golkilipa wake kutoka Argentina, Emiliano Martinez (27), anabakia klabuni hapo baada ya kujipanga kuimaliza safu yake ya langoni katika majira ya joto. ***(Mirror)***

**LEICESTER YAMTAKA JOVIC**
REAL Madrid iko tayari kujadili ofa mbalimbali kuhusiana na kumuuza mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Serbia, Luka Jovic (22), huku Leicester City ikiamini itamsajini nyota huyo kwa dau la pauni milioni 31. ***(Star)***

**MRITHI WA SANCHO ASAKWA**
MKURUGENZI wa Michezo wa Borussia Dortmund, Michael Zorc, amesema klabu hiyo ya Ujerumani inalazimika kuanza kuorodhesha nyota kwa ajili ya kuziba pengo la winga wa England, Jadon Sancho (20), ambaye ataondoka klabuni hapo katika majira ya joto. ***(Kicker - in German)***

**MADRID YAMPANGA MBAPPE**
REAL Madrid inajipanga kumsajili mshambuliaji Mfaransa, Kylian Mbappe (21), kutoka Paris St-Germain na kiungo wa Rennes, Eduardo Camavinga (17), ifikapo mwakani na wamewaambia wasikubali kusaini mikataba mipya. ***(Sport - in Spanish)***

**GIROUD ANUKIA INTER**
INTER Milan inataka kumsajili beki wa kushoto wa Timu ya Taifa ya Italia, Emerson Palmieri (25) na straika Mfaransa, Olivier Giroud (33), kutoka Chelsea. ***(Goal)***

**PELLISTRI AGOMBEWA ULAYA**
CHELSEA imeungana na Manchester City pamoja na Juventus katika mbio za kuwania saini ya winga wa Penarol, Facundo Pellistri (18). Nyota huyo wa Uruguay anamaliza mkataba wake na klabu hiyo ya Amerika ya Kusini ifikapo mwaka 2022. ***(Calciomercato, via Express)***

HABARI MICHEZO

# MASHABIKI WA SIMBA, YANGA WAENDELEA KUCHANGIA DAMU

Na Mary Geofrey

KUELEKEA mechi ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA, kati ya Simba na Yanga itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam, chupa 200 za damu zinatarajiwa kuchangwa kwa ajili ya kuwasaidia wagonjwa waliolazwa katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI).

Wadhamini wa klabu hizo mbili, Kampuni ya GSM kwa upande wa Yanga na Romario Sports, wanaoidhamini Simba, kwa pamoja wametoa jezi 200 kwa lengo la kuwapatia mashabiki wa timu hizo mbili ambao watajitokeza kuchangia damu katika taasisi hiyo.

Mhamasishaji wa mchakato huo, Gulam Dewji, alitangaza mpango huo jijini jana, wakati wakizungumza na waandishi wa habari kuhusu malengo na mikakati yake ya kusaidia kuokoa maisha ya Watanzania kupitia mechi za watani hao wa jadi.

Dewji alisema amekuwa akiguswa na changamoto ya upatikanaji wa damu kwa wagonjwa nchini, hivyo aliamua kuwashirikisha wadhamini wa timu hizo ambao walikubali kushiriki kwenye zoezi hilo litakalofanyika kuanzia leo.

"Tuliomba jezi 100 kwa Simba na 100 kwa Yanga, wote walitoa jezi hizo zenye thamani ya Sh. 15,000 kila moja, ambazo zitaanza kugaiwa kwa mashabiki wa timu hizo watakaojitokeza kuchangia damu kuanzia kesho (leo) hapa MOI," alisema Dewji.

Aliongeza malengo yake ni kuchangia chupa 1,000 za damu kwa kila mwezi na baadaye wataendelea na zoezi hilo katika mikoa mingine hapa nchini.

Pia aliwahamasisha mashabiki wa timu hizo kuvaa barakoa watakaposhiriki katika mtanange huo kwa ajili ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona.

Naye Mkurugenzi wa Uzalishaji wa GSM, Hersi Said, alisema wapo tayari kuendelea kudhamini mpango huo kwa ajili ya kuchangia wagonjwa wanaohitaji damu.

"Tulipopewa taarifa na Mzee Dewji hatukuchukua dakika 10 kukubali, tunaahidi pia kuendelea kutoa zaidi kwa ajili ya kusaidia wagonjwa wanaohitaji damu ikiwezekana kufika mikoani," alisema Said.

Mwakilishi wa Romarid Sports, Mussa Mwambajingu, aliwataka mashabiki wa timu zote mbili kujitokeza kuchangia damu na kupata jezi za klabu hizo wanazozishabikia.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Tiba MOI, Dk. Samweli Swai, mbali na kushukuru, alisema taasisi hiyo inahitaji chupa 30 hadi 40 kwa siku na chupa 900 hadi 1,000 kwa mwezi.

Aliwataja wahitaji wakubwa wa damu katika taasisi hiyo ni majeruhi wa ajali ambao wanalazimika kufanyiwa upasuaji wa mifupa mikubwa ya paja na upasuaji wa ubongo.



Wachezaji wa mpira wa kikapu kutoka sehemu mbalimbali jijini Dar es Salaam, wakifanya mazoezi kulinda viwango vyao kwenye Uwanja wa Jakaya Kikwete hivi karibuni. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# Azam yakanusha kumhitaji Matola

Na Saada Akida

LICHA ya kushindwa kufanya vema msimu huu, uongozi wa Azam FC, umesema hawana mpango wa kuvunja benchi la ufundi timu hiyo ambalo linaongozwa na Mromania, Aristica Cioaba.

Kocha huyo ambaye anasaidiwa na Mrundi Vivier Bahati, wameshindwa kutwaa taji la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu na kuvuliwa ubingwa wa michuano ya Kombe la FA.

Azam imelazimika kutoa kauli hiyo baada ya kuwapo kwa tetesi za kumwania Kocha Msaidizi wa Simba, Seleman Matola.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema jijini Dar es Salaam jana kuwa, hawana mpango wowote wa kufanya mabadiliko kwenye benchi la ufundi na makocha waliopo, wataendelea nao katika msimu ujao.

Popat alisema uongozi wa klabu hiyo bado unaimani na makocha hao na watawapa baraka za kuendelea na majukumu yao kwa ajili ya kuboresha kikosi hicho kuelekea msimu ujao.

"Taarifa kuhusu Matola hazina ukweli, Cioaba ataendelea kuwa kocha mkuu akisaidiwa na Bahati, hawa ndio wataendelea na mipango ya kujenga kikosi imara cha msimu ujao," alisema Popat.

Aliongeza kwa sasa wapo katika mchakato wa kutafuta kocha wa timu ya vijana kwa ajili ya kuchukua mikoba ya Bahati ambaye alipandishwa kwenda timu ya wakubwa.

## Polisi yatamba haishuki daraja

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Polisi, Yusuph Sape, amesema anajipanga vema kuhakikisha timu yake haishuki daraja licha ya kukabiliwa na mechi ngumu kwenye Ligi Kuu Zanzibar ambayo inaelekea ukingoni.

Sape alisema kauli hiyo baada ya kushinda mechi mbili za ugenini huko Pemba na sasa amebakiza michezo ya nyumbani (Unguja).

Kocha huyo alisema anatarajia kuendelea kufanya vizuri katika mchezo wake wa leo dhidi ya Kipanga, ingawa anaifahamu ni moja ya timu zenye vikosi imara kwenye ligi hiyo ya juu Zanzibar.

"Wakati tunaanza msimu huu, hatukufanya vizuri karibu michezo yote ya mwanzo tulipoteza, lakini hivi sasa tumerekebisha makosa mbalimbali ndani ya kikosi chetu na tunapata matokeo mazuri kila tunaposhuka dimbani, nguvu zetu zote ni kuhakikisha timu haishuki daraja," Sane alisema.

Hata hivyo aliwataka mashabiki wa Polisi kuendelea kuipa hamasa timu yao ili iweze kutimiza malengo yake wakati huu ambao kila klabu inapambana kutimiza malengo yake.

Polisi yenye pointi 32 kibindoni, ipo katika nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar inayoshirikisha timu 16 huku klabu sita zikitarajiwa kushuka daraja.

## Ngorongoro Marathon kufanyika Agosti

Na Shufaa Lyimo

WANARIADHA kutoka sehemu mbalimbali nchini watachuana katika mbio za Ngorongoro Marathon ambazo zimepangwa kufanyika Agosti 2, mwaka huu kwenye Wilaya ya Ngorongoro mkoani Arusha, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, mwanariadha maarufu nchini, Alphonce Simbu, alisema anaendelea vizuri na mazoezi kwa ajili ya kushiriki mbio hizo.

Simbu alisema anaamini mashindano hayo yataanza kurejesha viwango vya wanariadha ambao walikaa muda mrefu bila ya kushiriki michuano kutokana na janga la corona.

"Kwa upande wangu naendelea na mazoezi ili kuuweka mwili wangu sawa kuelekea mbio hizo, ninajituma sana kwa sababu nilikaa muda mrefu bila kushiriki mashindano yoyote," alisema Simbu.

Mwanariadha huyo alimewaomba Watanzania waendelee kuyaombea mataifa mengine ambayo bado wanachangamoto kubwa ya ugonjwa wa COVID 19 ili virusi vya ugonjwa huo vimalizike na maisha yao yaendelee kama zamani ikiwamo michezo.

"Tushirikiane kwa umoja wetu kuziombea nchi zote ambazo zinasumbuliwa na ugonjwa huo, tunahitaji kuona maisha mengine yaendelea, tuondokane na janga hili," alisema Simbu.

Michezo
Jumamosi Julai 11, 2020
Nipashe



Ibrahimovic hajui hatima yake Milan HABARI UK 22



Mshambuliaji wa Manchester United, Bruno Fernandes (kushoto), akiwania mpira dhidi ya beki wa Aston Villa, Tyrone Mings, katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa juzi usiku. United ilishinda mabao 3-0. **PICHA: MTANDAO**

## SIMBA QUEENS YAICHAPA YANGA

**Na Saada Akida**

SIMBA Queens imeendeleza ubabe kwa watani zao baada ya kuwafunga mabao 5-1 katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Simba Mo Arena.

Ushindi huo umeifanya Simba Queens kujiimarisha katika kilele cha msimamo wa ligi hiyo kwa kufikisha pointi 38 wakati watani zao Yanga Princess wamebakiwa na pointi 23.

Mabao ya Simba Queens katika mchezo huo yalifungwa na nahodha, Mwanahamisi Omary na Opa Clement kila mmoja alifunga magoli mawili huku lingine likiwekwa kimiani na kiungo wa kimataifa wa timu hiyo kutoka Burundi, Joelle Bukuru.

Bao la kufutia machozi la Yanga Princess katika mchezo huo wa mzunguko wa pili lilifungwa na Shelder Boniface.

Nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo ambayo kila timu imecheza mechi 15 inashikiliwa na mabingwa watetezi, JKT Queens yenye pointi 35 na Ruvuma Queens inafuata ikiwa na pointi 34.

# SIMBA SC, YANGA KUMALIZA TAMBO

●●●Mnyama ajipanga kuthibitisha ubora wake, huku Yanga wakiiota tiketi ya kushiriki michuano ya CAF......

**Na Somoe Ng'itu**

ZAIDI ya kisasi! ndivyo kila upande kati ya Simba na Yanga unavyosema kuelekea mechi yao ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA inayotarajiwa kuchezwa kesho Jumapili kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam.

Mwamuzi wa kati wa mechi hiyo itakayochezwa kuanzia saa 11:00 jioni, atakuwa ni Aboubakari Mturo, ambaye atasaidiwa na Abdallah Mwinyimkuu, Nadeem Aloyce, Ramadhani Kayoko, Frank Komba na Kassim Mpanga huku Kamisaa akiwa ni Ally Katolila.

Mechi hiyo itakuwa ni ya tatu kuwakutanisha msimu huu baada ya mchezo kutoka sare ya mabao 2-2 katika mchezo wa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara, na waliporudiana Machi 8, mwaka huu, Yanga ilipata ushindi wa bao 1-0.

Hata hivyo, mbali na kusaka heshima, mechi ya kesho ni mchezo wa mashindano yanayochezwa kwa mfumo wa mtoano na bingwa wake hupata tiketi ya kuiwakilisha Tanzania Bara kwenye michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika (CAF).

Simba ilifika hatua hiyo baada ya kuwaondoa waliokuwa mabingwa watetezi wa michuano hiyo Azam FC kwa kuwafunga mabao 2-0, wakati Yanga ilisonga mbele kutokana na kuichapa Kagera Sugar magoli 2-1, mechi zote za hatua ya robo fainali zikichezwa jijini.

Licha ya Ligi Kuu Tanzania Bara kuwa haijamalizika, mabingwa wa msimu huu, Simba watashuka dimbani tayari wakiwa na tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ambayo yanasimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenvroeck, alisema amejiandaa kukamilisha msimu wa 2019/20 vizuri na anaamini kikosi chake hakitarudia makosa yaliyofanywa kwenye mchezo uliopita. Sven alisema anajua mechi hiyo ni ngumu na ndio tegemeo pekee kwa wapinzani wao Yanga kupata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa msimu ujao.

Alisema wanahitaji kuongeza umakini na kucheza katika kiwango chao bora ili wapate matokeo chanya na hatimaye kuwaondolea machungu mashabiki wao wanaoumizwa na kipigo walichapata Machi 8, mwaka huu kutoka kwa watani zao.

"Tunahitaji kuwa makini na watulivu zaidi, mechi ya Jumapili ni mechi itakayokuwa na ushindani, changamoto mbalimbali pamoja na presha, tunatakiwa kutokuwa na papara, tunachotakiwa kufanya ni kutumia vema nafasi tutakazozitengeneza," Sven alisema.

Naye Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema wamejipanga kupata ushindi ili kuendelea na kampeni yao ya kuchukua vikombe msimu huu.

Manara alisema siri ya mafanikio ya timu yao msimu huu, imetokana na kuwa na kikosi imara ambacho kwa asilimia kubwa kitaendelea kuitumikia klabu hiyo tena katika msimu ujao.

"Tumejipanga, watatueleza walipataje ushindi Machi 8, au kama watabahatisha kwa mara nyingine, hawawezi," Manara alitamba.

Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael, aliliambia gazeti hili mechi ya kesho kwake ni muhimu zaidi kuliko mechi nyingine walizocheza msimu huu.

Eymael alisema si kama wanahitaji kuendelea kuifunga Simba, lakini wanahitaji kusonga mbele katika mashindano hayo ili watimize malengo ya kukichukua kikombe hicho na kupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa.

"Ni mechi muhimu sana kwa Yanga, ni mechi ambayo itatupa mwelekeo wa kushiriki mashindano ya kimataifa, tunahitaji kushiriki mashindano ya CAF msimu ujao, hii ndio nafasi pekee tuliyonayo ili kufikia malengo, hatutaki kumaliza msimu huu bila kikombe, baada ya kupoteza taji la Ligi Kuu," Eymael alisema.

Mbelgiji huyo amewataka mashabiki wa Yanga kutokuwa na hofu na kuendelea kuungana ili wapate ushindi.

Mechi nyingine ya hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo itachezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga kati ya wenyeji Sahare All Stars dhidi ya Namungo FC kutoka Lindi.

Fainali za mashindano hayo zitafanyika Agosti 2, mwaka huu kwenye Uwanja wa Nelson Mandela ulioko Sumbawanga, mkoani Rukwa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >